Jumatano Juni 1, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580963

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US

SportPesa

JACKPOT BABA LAO!

TZS. 233,880,320

CHEZA SASA KWA 1000/= TU!

SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Ukivaa** kimini, mlegezo faini mifuko mitano ya saruji

UKURASA 3



**SIMBA YAMTIMUA PABLO, AKATAA KUPOKEA BARUA**

UKURASA 24

# Bil. 100/- za Samia zashusha bei ya mafuta

• **Matumaini** zaidi unafuu yaja, wengi wafurahia... *Ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akipokea Kombe la Dunia kwa Balozi wa kombe hilo, kutoka Shirikisho la Mpira wa Miguu Duniani (FIFA) ambaye ni mchezaji wa zamani wa Timu ya Taifa ya Brazil, Juliano Belletti, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 7

**WATAKA MWENDOKASI KUTUMIKA SABASABA**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, imeiagiza Wakala wa...

## Rais Mwinyi abariki nauli boti kupanda

UKURASA 3

# 'Nondo' 12 Mambo ya Nje kuipaisha Tanzania

- KUTAFUTA MIKOPO NAFUU
- MASOKO YA NJE KWA AJILI YA BIDHAA ZA TANZANIA
- AJIRA ZA WATANZANIA KIMATAIFA
- KUVUTIA UWEKEZAJI, KUIMARISHA DIPLOMASIA YA UCHUMI
- KISWAHILI KUPIGIWA DEBE



UKURASA 2

MICHEZO SIMBA SC YAMTIMUA PABLO UK.24 MAONI, KATUNI UK.6



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, akiwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Bil. 100/- za Samia zashusha mafuta

**Na Waandishi Wetu**

SHILINGI bilioni 100 zilizotolewa na Rais Samia zimeshusha bei za mafuta kuanzia bei mpya zitakazotumika kuanzia leo. Hivyo ndiyo inavyoweza kuelezwa kutokana na bei mpya zilizotangazwa jana.

Baada ya kupanda kwa mafuta yaliyoanza kutumika mwezi uliopita, serikali ilianza kuchukua hatua mbalimbali ili kupunguza makali ya bei za bidhaa hizo ikiwamo kutolewa kwa ruzuku ya Sh. bilioni 100.

Kutokana na hakli hiyo, hatimaye bei mpya za petroli na dizeli zilizotangazwa jana na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) zimeshuka hali ambayo itawapa unafuu wananchi.

Taarifa iliyotolewa jana na EWURA ilibainisha kuwa bei hizo ni kwa shehena zinazoingia katika bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara.

Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa EWURA, Titus Kaguo, alisema kwa Dar es Salaam, petroli imeshuka kwa Sh. 306 kwa lita; Mtwara Sh. 282 na Tanga kwa Sh. 152 mtawalia.

Wakati hali ikiwa hivyo kwa petroli, Kaguo alisema dizeli imeshuka kwa Sh. 320 kwa lita kwa Dar es Salaam, Sh. 476 kwa Tanga na Sh. 486 kwa mafuta yanayoingia kupitia Bandari ya Mtwara.

"Kutokana na kushuka huko, kwa Dar es Salaam bei ya petroli kwa lita itakuwa Sh. 2,994 badala ya Sh. 3,301 kwa lita. Bei mpya ya dizeli itakuwa Sh. 3,131 badala ya Sh. 3,452 kwa lita," alisema Kaguo. Kwa mafuta yanayoshushwa kupitia Bandari ya Tanga, Kaguo alisema bei mpya ya petroli itakuwa Sh. 2,985 kutoka Sh. 3,137 wakati dizeli itakuwa Sh. 3,162 kutoka Sh. 3,639 kwa lita iliyokuwapo awali.

Aidha, katika Bandari ya Mtwara, alisema petroli itauzwa Sh. 2,979 kutoka Sh. 3,262 kwa lita wakati bei ya dizeli itakuwa Sh. 3,165 kutoka Sh. 3652 kwa lita.

"Bei hizi zilizotajwa hapa ni kwa ile miji ambayo bandari huzika zipo na shehena ya bidhaa hizo zinashushwa. Kwa hiyo hadi kufika kwenye miji husika kutoka kwenye eneo la bandari bei itakuwa inapanda kutokana na gharama za usafirishaji lakini kutakuwa na unafuu wa wastani wa bei zilizotajwa kutokea kwenye chanzo cha shehena," alisisitiza Kaguo.

**TPDC KULETA MAFUTA**

Katika hatua nyingine, Kampuni ya Vitol Bahrain E.C imeshinda zabuni tatu za usafirishaji wa mafuta huku ikiwashangaza Wakala wa Serikali wa Uagizaji wa Mafuta ya Pamoja (PBPA) kwa zabuni ya mafuta ya nne ambayo itaisafirisha kwa bei sawa na bure.

Vilevile, Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) kwa mara ya kwanza limeshinda zabuni ya usafirishaji wa mafuta ya dizeli kuanzia Julai mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa PBPA na Mwenyekiti wa Kamati ya Zabuni ya Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja, Ali Saeed, alisema wamefungua zabuni ya Julai na wenye zabuni wamefika na kuingiza zabuni zao kwenye kasha na kufunguliwa hadharani.

Alisema kampuni saba zimeshiriki katika zabuni hizo na kampuni ya Tanzania iliyoshiriki ni TPDC na baada ya kutangazwa zabuni ya kwanza, kamati inachambua nyaraka kuhakiki kama imekamilisha masharti ya zabuni yenyewe.

Saeed alisema kama amekamilisha wanatangaza mshindi wa kiwango cha chini. Dizeli yenye ujazo wa 100,857 ambaye ameshinda Vitol Bahrain kwa bei ya chini na ametimiza vigezo vyote vya uagizaji wa mafuta kwa pamoja.

Mjumbe wa Kamati ya Kutathmini Zabuni, Paulo Runyalula, alisema tathmini inafanana na wastani wa mwezi uliopita, akifafanua: "Mafuta ya Julai yatakuwa wastani wa mafuta ya bei ya Juni, sasa tunachowashindanisha ni gharama za kusafirisha mafuta pamoja na faida yao."

Alibainisha kuwa washiriki walikuwa wanne: TPDC, Vitol Bahrain E.C, Agusta na Sahara, akisema: "Aliyeshinda kwa Dola za Kimarekani 46.4 ambaye ataleta tani 100,857 na tenda ya pili ya dizeli ameshinda Vitol Bahrain na tenda ya tatu ya dizeli ameshinda TPDC.

"Sasa hii kampuni ya Vitol Bahrain imeshinda zabuni ya nne gharama ya kusafirisha mafuta Dola za Marekani 0.05 kwa huo mzigo wa tani 100,857 utaletwa kama kwa Dola za Marekani 5,700, ni sawa na bure," alisema.

**WACHUMI WAFUNGUKA**

Mtaalamu wa Uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Prof. Razack Lukina, alisema kushuka kwa bei ya mafuta kutapunguza ukali wa maisha kwa kuwa wafanyabiashara watashusha bei za vitu vilivyopanda kutokana na kupanda kwa bei ya nishati hiyo.

"Wafanyabiashara walipandisha bei za bidhaa kwa sababu gharama za mafuta zilipanda. Kwa hiyo, kama kesho yanashuka, tunatarajia vitu vishuke bei. Siwezi kukuhakikishia hilo lakini ingetakiwa iwe hivyo," alisema.

Mchumi huyo aliitaka serikali kusimamia bei za bidhaa hizo kuhakikisha kuwa zinashuka kwa kuwa wafanyabiashara wanatabia ya kutoshusha bei hizo hata pale tatizo lililosababisha likitatuliwa.

"Ni 'nature' (asili) ya wafanyabiashara kutoshusha bei ya bidhaa sasa hapo serikali inatakiwa isimamie ili ishuke, ni suala la kuona bei kwanza inashuka kisha tutaona namna gani serikali itasimamia hilo," alisema.

Profesa wa Uchumi, Samwel Wangwe, alisema kushuka huko kwa bei ya mafuta kutachochea shughuli za maendeleo kwa kuwa mafuta yamekamata sehemu zote muhimu kwa maendeleo.

"Mafuta yanaingia kwenye sekta nyingi, kilimo kwenye matrekta, viwanda... Kwa hiyo, gharama zikiwa ndogo, sekta hizo zitajiendesha kwa wingi na hivyo kupunguza mfumuko wa bei. Bei nazo zikipungua ina maana mwananchi wa kawaida atamudu gharama za bidhaa," alisema.

Bei ya mafuta kwa kila sehemu kulingana na mabadiliko yaliyotangazwa zinapatikana ukurasa wa 4 na 5.

***Imeandikwa na Beatrice Shayo na Jenifer Gilla**

# 'Nondo' 12 za Mambo ya Nje kuipaisha nchi

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WIZARA ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imebainisha vipaumbele vyake 12 katika mwaka wa fedha 2022/23 ikiliomba Bunge iidhinishe Sh. bilioni 208.3 ili kuvitekeleza.

Kati yake, limo suala la kutafuta mikopo ya gharama nafuu, masoko, ajira za Watanzania, kuvutia uwekezaji na kutekeleza diplomasia ya uchumi.

Akiwasilisha jana bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/23, Waziri wake, Balozi Liberata Mulamula, alisema wameweka kipaumbele katika kutekeleza majukumu mbalimbali.

Aliyataja majukumu hayo wanayokwenda kuyatekeleza kuwa ni pamoja na kuendelea kulinda na kutetea misingi ya Taifa ndani na nje ya nchi.

Waziri huyo alisema wataendelea kutekeleza diplomasia ya uchumi ikiwa ni pamoja na kuwezesha Balozi kuwa kiungo muhimu katika kuvutia uwekezaji.

"Kutafuta masoko ya bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini; kutafuta misaada na mikopo yenye masharti nafuu na kutafuta fursa za ajira na masomo kwa Watanzania nje ya nchi," alisema.

Alitaja vipaumbele vyao vingine ni kuendelea kuimarisha uhusiano na nchi nyingine na jumuiya za kimataifa; kutangaza na kuhamasisha matumizi ya lugha ya Kiswahili nje ya nchi; na kuweka mazingira wezeshi na kuhamasisha ushiriki wa Watanzania wanaoishi nje katika kuchangia maendeleo ya nchi.

"Sita; ni kuendelea kushiriki katika juhudi za kulinda na kuimarisha amani duniani na maendeleo kupitia Umoja wa Mataifa, pia kuendela kushiriki kikamilifu katika kuimarisha mtangamamo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu utekelezaji wa majukumu ya wizara, masuala ya uhusiano wa kimataifa na mtangamano wa kikanda," alisema.

Balozi Mulamula alitaja kipaumbele chao cha tisa ni kuendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu ya taasisi zilizopo chini ya wizara, pia kuendeleza viwanja vinavyomilikiwa na serikali nje ya nchi na kukarabati majengo ya balozi ili kupunguza gharama na kuchangia mapato ya serikali.

Alisema kipaumbele chao cha 11 ni kuendelea kubaini maeneo mapya kimkakati kwa lengo la kunufaika na fursa zilizopo kwa maslahi mapana ya Taifa na cha mwisho ni kuendelea kusimamia rasilimali watu na fedha makao makuu ya wizara na balozini.

**MALENGO YA TAASISI**

Balozi Mulamula alisema katika mwaka 2022/23, Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC) kimepanga kukusanya mapato ya Sh. milioni 16.7 kutokana na vyanzo vya ndani.

"Mapato hayo yatatumika kugharamia uendeshaji wa kituo, 110 mishahara na ununuzi wa vifaa tiba na mradi ya maendeleo ya ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje katika Hospitali ya AICC na kinakamilisha taratibu za kuanza ujenzi wa kituo cha mikutano kitakachoitwa Mount Kilimanjaro International Convention Centre jijini Arusha," alisema.

Waziri huyo alisema Chuo cha Diplomasia kimepanga kukusanya Sh. bilioni 3.6 kutoka katika vyanzo vya ndani.

Alisema Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Masuala ya Demokrasia na Utawala Bora (APRM) unatarajia pamoja na majukumu mengine kuendelea kufanya tathmini katika masuala ya demokrasia na siasa, usimamizi wa uchumi, uendeshaji wa mashirika ya biashara na utoaji wa huduma za jamii.

**KUPUNGUA MADUHULI**

Alisema katika kipindi cha Julai, mwaka jana hadi Aprili, mwaka huu, wizara imekusanya Sh. milioni 854.3 sawa na asilimia 33 ya lengo lililopangwa kwa mwaka 2021/22, akifafanua kuwa kupungua kwa mapato hayo kumetokana na kukosekana kwa wapangaji katika baadhi ya majengo ya serikali kwenye balozi za Tanzania nje ya nchi.

"Hali hii imesababishwa na uwapo wa janga la UVIKO-19 uliosababisha biashara nyingi katika nchi mbalimbali kufungwa. Fedha zote za maduhuli zilizokusanywa ziliingizwa kwenye mfuko mkuu wa serikali," alisema.

**MAJENGO YA BALOZI**

Alisema wizara inaendelea na mazungumzo na CRDB kuhusu ushirikiano katika ujenzi wa majengo ya ofisi, vitega uchumi na makazi ya watumishi balozini.

Waziri huyo pia alisema pamoja na kuwapo mafanikio ya kiutendaji katika kutekeleza bajeti ya mwaka 2021/22, wizara ilikabiliwa na matatizo ya upungufu wa watumishi.

Alisema wizara inaendelea kuwasiliana na mamlaka za ajira kwa ajili ya kupata vibali vya ajira mpya na ajira mbadala.

Alisema katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya mikataba na hati 32 za makubaliano ya ushirikiano zilisainiwa.

**KAMATI YA BUNGE**

Akiwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mjumbe wa Kamati hiyo, Zahor Mohammed Haji, alisema matokeo ya ukaguzi wa mradi wa maendeleo yanaonyesha hadi Machi mwaka huu, walipotembelea hakukuwa na mradi uliotekelezwa.

"Sababu za kuchelewa kuanza kwa mradi wa kuimarisha miundombinu ya Chuo cha Diplomasia ni kuwapo kwa matatizo ya kimkataba baina ya chuo na mkandarasi.

"Kamati ilielezwa utekelezaji wa mradi wa ofisi na majengo ya kitega uchumi wa ofisi za ubalozi wa Tanzania Kinshasa haujaanza kutokana na kutokamilika kwa taratibu za ununuzi na kutofanya tathmini za kihandisi," alisema.

Mjumbe huyo alisema kamati ililezwa viwanja ambavyo nyumba za makazi za Balozi wa Tanzania Addis Ababa zingejengwa lakini Tanzania ilinyang'anywa umiliki wa viwanja hivyo na mamlaka za Ethiopia kutokana na kushindwa kuviendeleza.

# Rais Mwinyi abariki nauli za boti kupanda

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema kuwa serikali imeridhia kupanda kwa nauli ya boti kutoka Sh. 25,000 hadi 30,000 (kwa usafiri wa daraja la chini) kutoka Zanzibar hadi Dar es Salaam.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo Ikulu Zanzibar, katika mkutano na waandishi wa habari, ikiwa ni mwendelezo wa utaratibu wake wa kukutana na wahariri na waandishi wa habari kila mwisho wa mwezi.

Alisema uamuzi huo umefikiwa kwa kuzingatia maombi ya muda mrefu ya wamiliki wa vyombo hivyo, (takriban miaka saba), huku bei ya mafuta ikipanda katika kipindi hiki.

"Tumeongeza bei ya nauli ya boti kwa shingo upande kutokana na kupanda kwa gharama ya bei ya mafuta, lakini bei ya mafuta itakaposhuka tutaangalia uwezekano wa kushusha bei ya usafiri huo," alisema Dk. Mwinyi.

Alisema kupanda kwa bei ya mafuta na bidhaa zingine kunatokana na kupanda kwa mfumuko wa bei duniani kulikotokana na vita vya Ukraine na Russia ambako mafuta mengi yanatoka nchini huko.

Pia Dk. Mwinyi alisisitiza matumizi ya mashine ya EFD katika ukusanyaji kodi na kuwataka wananchi kudai risiti wanapofanya ununuzi, ili kuiwezesha serikali kukabiliana na hali ya kiuchumi.

Alisema katika kukabiliana na athari zilizotokana na misukosuko ya kiuchumi duniani, serikali imelazimika kupunguza kiwango cha ushuru pamoja na kufidia viwango vya bei za bidhaa, akabainisha umuhimu wa kukusanya kodi na kusisitiza matumizi ya EFD na wananchi kudai risiti wakati wanapofanya ununuzi.

Alizitaka mamlaka zinazohusika kuchukua hatua stahiki kwa wananchi wasiolipa ushuru kupitia mashine hizo za VFB.

Hata hivyo, alisema kuna umuhimu kwa wananchi wa Zanzibar kuongeza uzalishaji wa kilimo cha karafuu, kwa kigezo kuwa pamoja na misukosuko ya kiuchumi duniani, zao hilo limebaki kuwa na bei nzuri katika soko la Dunia (Dola 7,500 kwa tani), kiasi ambacho kimeiwezesha serikali kuwalipa wakulima kiwango cha bei za kawaida.

Akizungumzia upandishaji wa mishahara kupitia sekta binafsi, Dk. Mwinyi, alisema serikali inakusudia kukaa pamoja na waajiri wa sekta hiyo ili kuona namna ya kuwapandishia mishahara wafanyakazi wao ili waweze kumudu gharama za maisha.



Kuhusu changamoto ya uharibifu wa mazingira unaovikabili visiwa vya Unguja na Pemba, Dk. Mwinyi alisema kuna tatizo kubwa husussan katika suala la uchimbaji wa mawe, mchanga pamoja na ukataji mikoko na kubainisha kuwapo kwa mikakati ya kuikabili hali hiyo.

Aliwahakikishia wananchi kisiwani Pemba ambao maeneo yao yalipimwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Chake-Wete na kubainika kutokuwa na matatizo, kuwa watalipwa mara moja.

# Ukivaa nguo fupi, mlegezo faini mifuko mitano saruji

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

VIONGOZI Kata ya Tandala, wilayani Makete, Mkoa wa Njombe, kupitia vikao vya kata (KAMAKA), wametunga sheria ndogo ya kuwakamata wanawake wanaovaa nguo fupi, zinazochora maumbile yao pamoja na wanaume wanaovaa suruali chini ya makalio na kuwapiga faini ya mifuko mitano ya saruji itakayojenga miradi ya kata.

Mtendaji wa kata hiyo, Maximilian Msigwa, alisema uamuzi huo umefanyika ili kudhibiti mavazi yasiyofaa katika jamii na baadhi ya watu wameshakamatwa.

"Tumekuwa na mabinti wengi wanaokuja kutafuta riziki kwa njia tofauti, sasa wanapokosea lazima tuwanyooshe warudi kwenye mstari, akikamatwa analipishwa mifuko mitano ya saruji kwa ajili ya ujenzi, kwasababu tuna ujenzi wa shule yetu ya msingi Tandala," alisema Msigwa.

Alisema kabla ya kuanza kwa zoezi hilo wamiliki wa sehemu za starehe na wananchi kwa ujumla walipewa taarifa kwa ajili ya kujirekebisha kabla sheria hiyo haijaanza kufanya kazi na kuongeza kuwa wote wanaoshindwa kulipa gharama hizo kumewekwa utaratibu wa kuzungumza na viongozi wao wa vijiji ili kuwatambua na kuwarudisha kwao.

Lususu Mbilinyi na Maulo Sanga ni baadhi ya wananchi wa Kata ya Tandala, ambao wamepongeza uamuzi huo huku wakitaka sheria hiyo isimamiwe ipasavyo katika kulinda maadili ya Mtanzania.

"Sheria hii inapaswa kusimamiwa ili iweze kuwa na maadili maana vijana wengi wa sasa wanavaa hovyo kwa kigezo cha utandawazi hii haikubaliki lazima maadili yafuatwe kwa kizazi cha sasa na baadaye," alisema Maulo Sanga.

Sanga, aliwaomba mafundi cherehani wasikubali kushona nguo fupi na zisizofaa katika jamii kwa kuwa zinaweza kuwaharibia kazi zao na kuwa miongoni mwa wanaosababisha suala hilo kuzidi kukua nchini.




VisionFund TANZANIA MICROFINANCE BANK LTD

## VISIONFUND TANZANIA MICROFINANCE BANK LTD
## VACANCIES

VisionFund Tanzania Microfinance Bank Ltd (VFT MFB) formerly known as SEDA is a fast growing and reputable Micro Finance Bank (MFB), has a loan book of TZs. 17 billion and 30,000 customer base, more that 5,000 of them being small holder farmers. VFT-MFB is seeking to employ a dynamic and committed Tanzanian young men & women who have passion for people's economic development to fill in the vacant position detailed here below;

**Work reference no. 008/22**
**Position: SME/Individual Lending Manager**
**Reporting to: Chief Operations Officer**

**Responsibility:**
- Staff Recruitment and Training on Well-equipped staff for Individual Lending
- Monitoring on Portfolio Growth through Individual Lending
- Coordinate the efficiency and harmony among stakeholders of the Individual Lending Methodology
- Reporting - Real time and reliable information made available for different stakeholders
- Market Surveys and Lesson Learnt - Understanding the outcomes of the Individual Loan Product and to know the areas of improvement and the new opportunities in the market

**Main tasks:**
- To supervise the Individual Loan activities ensuring that financial and operational performance targets for the Individual Loan Product are achieved through specialized Loan Officers and their Supervisors.
- To train Loan Officers and Supervisors on the marketing and selling of the Individual Loan Product
- To develop and foster a career path for Individual Lending Loan Officers and Loan Supervisors
- To continuously train BCMs for effective monitoring of the Individual Loan Product
- To provide guidance on the lending business plan and performance targets
- Monitoring the implementation of best practice, policies and procedures on Individual Lending
- Guidance on key result areas, implementation of activities, and workload
- Reporting on the progress of the Individual Loan Product to the management and other stakeholders.

**Education/Experience:**
- University Degree in Economics, Accounting, Finance, or Business Administration.
- Master's Degree in the related field will be an added advantage
- Minimum of 5 years of Individual/SME/Commercial Banking, Sales and Management.
- At least 3 years' experience in training and coaching SME/Individual lending teams.
- Advanced knowledge of related statutory and regulatory banking compliance regulations,
- Very good analytical skills (including the use of excel in analyzing data and reporting

**Mode of Application:**
Interested and suitably qualified individuals should forward their application letter, attaching copies of their academic and professional certificates; detailed CV's with three referees to: **vftHRstaff@vftz.co.tz**.
The position should be the subject of the email application.

**OR; through the postal address below:**

**The Chief Executive Officer,**
**VisionFund Tanzania Microfinance Bank Limited,**
**P.O. Box 1546,**
**Arusha TANZANIA.**

The application should reach the undersigned not later than **10th June 2022.**

N.B. Only short-listed candidates will be contacted

**Disclaimer**
VisionFund Tanzania Microfinance Bank would like to inform the general public that it has not engaged any consultant/agent to conduct recruitment on its behalf.

216881602

Arusha International Conference Center (AICC),
Serengeti Wing, Fifth Floor, Afrika Mashariki Road

THE MICROFINANCE SUBSIDIARY OF WORLD VISION

P.O. Box 1546 Arusha, Tanzania
T +255 27 2050143, 2050147
E info@vftz.co.tz | www.vftz.co.tz

TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)


# KUMB: PPR/2022 - 06/1

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 1 JUNI 2022

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 1 Juni 2022.**

Bei za mafuta katika soko la dunia zimeongezeka zaidi kutokana na, pamoja na mambo mengine, vita inayoendelea kati ya Urusi na Ukraine iliyoanza mwishoni mwa mwezi Februari 2022. Hii ilisababisha kuharibika kwa mfumo wa usambazaji wa mafuta kutokana na vikwazo vilivyowekwa dhidi ya Urusi na hivyo kuongezeka kwa bei za mafuta ghafi. Kwa kipindi cha mwezi Machi 2021 mpaka mwezi Machi 2022, bei ya chini ilikuwa dola za kimarekani 60.27 kwa pipa kwa mwezi Machi 2021 na bei ya juu ilikuwa dola za kimarekani 139.13 kwa pipa kwa mwezi Machi 2022, hivyo kusababisha bei katika soko la ndani kuongezeka kwa kiwango kikubwa.

**Mchoro hapo chini unaonesha Mwenendo wa Bei za Mafuta Ghafi katika Soko la Dunia kuanzia mwezi Machi 2021 Mpaka mwezi Machi 2022.**




Serikali ya Tanzania imechukua hatua mbali mbali katika kukabiliana na ongezeko kubwa la bei za mafuta nchini na kuhakikisha kunakuwepo na mafuta muda wote na hivyo kupunguza madhara kwa wananchi. Mnamo mwezi Mei 2022, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alitoa ruzuku ya shilingi billioni 100 katika harakati za kukabiliana na ongezeko la bei za mafuta katika soko la ndani kwa mwezi Juni 2022.

**Ruzuku ya shilingi billioni 100 imesaidia kupunguza bei za mafuta kama ifuatavyo:**

a) Bandari ya Dar es Salaam, petroli imeshuka kwa shilingi 306 kwa lita wakati dizeli imeshuka kwa shilingi 320 kwa lita.

b) Bandari ya Tanga, petroli imeshuka kwa shilingi 152 kwa lita na dizeli kwa shilingi 476 kwa lita.

c) Bandari ya Mtwara, petroli imeshuka kwa shilingi 282 kwa lita na dizeli kwa shilingi 486 kwa lita.

Hatua zilizochukuliwa na Serikali zimesaidia kupunguza ongezeko la bei ya mafuta kwa mwezi Juni 2022. Jedwali Na. 1 linaonesha tofauti ya bei za Mafuta katika vituo kabla na baada ya Ruzuku

**Jedwali Na.1 Bei za Mafuta kwa mwezi Juni 2022 kabla na baada ya ruzuku shilingi/lita**

| Bandari | Juni 2022 Bei kabla ya ruzuku | | | Juni 2022 Bei baada ya ruzuku | | | Kiwango cha Ruzuku | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
| Dar es Salaam | 3,301 | 3,452 | 3,299 | 2,994 | 3,131 | 3,299 | 306 | 320 | 0 |
| Tanga | 3,137 | 3,639 | | 2,985 | 3,162 | | 152 | 476 | 0 |
| Mtwara | 3,262 | 3,652 | | 2,979 | 3,165 | | 282 | 486 | 0 |

Kutokana na mgao wa ruzuku hiyo bei za Mafuta zimeshuka kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na.2.

**Jedwali Na. 2 Bei za Mafuta za rejareja kuanzia tarehe 1 Juni 2022**

| Bandari | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 2,994 | 3,131 | 3,299 |
| Tanga | 2,985 | 3,162 | 0 |
| Mtwara | 2,979 | 3,165 | 0 |

**Katika kutekeleza bei hizi, wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta watatakiwa kuzingatia yafuatayo: -**

(a) EWURA inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli kwa eneo husika zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba *152*00# na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.

(b) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, kifungu namba 166, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.

(c) Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (Price cap) au kushuka chini ya bei iliyoruhusiwa (Floor Price) kama ilivyokokotolewa kwa kutumia fomula na Kanuni za EWURA za Kupanga Bei za Mafuta za Mwaka 2022 zilizotangazwa kupitia Magazeti ya Serikali Na. 2A na 57 ya tarehe 3 Januari 2022 na 28 Januari 2022, sawia.

(d) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.

(e) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (Electronic Fiscal Pump Printers) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya mafuta ya petroli.

(f) Wauzaji wa Mafuta ya petroli wa rejareja watatakiwa kuuza Mafuta kwa kutumia bei yenye ruzuku kama inavyooneshwa kwenye Jedwali A. Kwa yoyote atakayekiuka AGIZO atachukuliwa hatua kali.

(g) Wauzaji wa Mafuta ya petroli wa jumla watatakiwa kuuza Mafuta kwa kutumia bei yenye ruzuku kama inavyooneshwa kwenye Jedwali B. Kwa yoyote atakayekiuka AGIZO atachukuliwa hatua kali.

# TANGAZO

## JEDWALI A: BEI ZA REJAREJA (Shs/Lita)

| Mji | Bei za Petroli bila ruzuku | Bei za Petroli baada ya ruzuku | Bei ya Dizeli kabla ya ruzuku | Bei za Dizeli baada ya ruzuku | Bei za Mafuta |
|---|---|---|---|---|---|
| **Dar es Salaam** | **3,301** | **2,994** | **3,452** | **3,131** | **3,299** |
| **Arusha** | **3,194** | **3,042** | **3,696** | **3,219** | **3,383** |
| Arumeru (Usa River) | 3,194 | 3,042 | 3,696 | 3,219 | 3,383 |
| Karatu | 3,212 | 3,060 | 3,714 | 3,237 | 3,402 |
| Longido | 3,205 | 3,053 | 3,707 | 3,230 | 3,394 |
| Monduli | 3,200 | 3,047 | 3,701 | 3,224 | 3,389 |
| Monduli-Makuyuni | 3,204 | 3,052 | 3,706 | 3,229 | 3,394 |
| Ngorongoro (Loliondo) | 3,279 | 3,126 | 3,781 | 3,303 | 3,475 |
| **Coast (Kibaha)** | **3,305** | **2,998** | **3,456** | **3,135** | **3,304** |
| Bagamoyo | 3,312 | 3,005 | 3,463 | 3,142 | 3,310 |
| Bagamoyo (Miono) | 3,343 | 3,036 | 3,494 | 3,173 | 3,341 |
| Chalinze Junction | 3,315 | 3,008 | 3,466 | 3,145 | 3,313 |
| Chalinze Township (Msata) | 3,319 | 3,012 | 3,470 | 3,149 | 3,318 |
| Kibiti | 3,321 | 3,014 | 3,472 | 3,151 | 3,320 |
| Kisarawe | 3,308 | 3,001 | 3,459 | 3,138 | 3,306 |
| Mkuranga | 3,311 | 3,004 | 3,462 | 3,141 | 3,309 |
| Rufiji | 3,328 | 3,022 | 3,479 | 3,158 | 3,327 |
| **Dodoma** | **3,360** | **3,053** | **3,511** | **3,190** | **3,358** |
| Bahi | 3,367 | 3,060 | 3,518 | 3,197 | 3,365 |
| Chamwino | 3,355 | 3,048 | 3,506 | 3,185 | 3,353 |
| Chemba | 3,386 | 3,079 | 3,537 | 3,216 | 3,385 |
| Kondoa | 3,392 | 3,085 | 3,543 | 3,222 | 3,391 |
| Kongwa | 3,357 | 3,050 | 3,508 | 3,187 | 3,355 |
| Mpwapwa | 3,361 | 3,054 | 3,512 | 3,191 | 3,359 |
| Mpwapwa (Chipogoro) | 3,373 | 3,066 | 3,524 | 3,203 | 3,371 |
| Mtera (Makatopora) | 3,379 | 3,072 | 3,529 | 3,208 | 3,377 |
| Mvumi | 3,366 | 3,059 | 3,517 | 3,196 | 3,365 |
| **Geita** | **3,466** | **3,159** | **3,617** | **3,296** | **3,465** |
| Bukombe | 3,455 | 3,148 | 3,606 | 3,285 | 3,454 |
| Chato | 3,487 | 3,180 | 3,638 | 3,317 | 3,486 |
| Mbogwe | 3,504 | 3,197 | 3,655 | 3,334 | 3,503 |
| Nyang'hwale | 3,481 | 3,174 | 3,632 | 3,311 | 3,480 |
| **Iringa** | **3,365** | **3,058** | **3,516** | **3,195** | **3,363** |
| Ismani | 3,370 | 3,063 | 3,521 | 3,200 | 3,369 |
| Kilolo | 3,369 | 3,062 | 3,520 | 3,199 | 3,368 |
| Mufindi (Mafinga) | 3,375 | 3,068 | 3,526 | 3,205 | 3,373 |
| Mufindi (Igowole) | 3,384 | 3,077 | 3,535 | 3,214 | 3,382 |
| **Kagera (Bukoba)** | **3,516** | **3,209** | **3,667** | **3,346** | **3,515** |
| Biharamulo | 3,491 | 3,184 | 3,642 | 3,321 | 3,489 |
| Karagwe (Kayanga) | 3,533 | 3,226 | 3,684 | 3,363 | 3,531 |
| Kyerwa (Ruberwa) | 3,539 | 3,232 | 3,689 | 3,368 | 3,537 |
| Muleba | 3,516 | 3,209 | 3,667 | 3,346 | 3,515 |
| Ngara | 3,504 | 3,197 | 3,655 | 3,334 | 3,503 |
| Misenyi | 3,525 | 3,218 | 3,676 | 3,355 | 3,523 |
| **Katavi (Mpanda)** | **3,466** | **3,159** | **3,617** | **3,296** | **3,464** |
| Mlele (Inyonga) | 3,443 | 3,136 | 3,594 | 3,273 | 3,442 |
| Mpimbwe (Majimoto) | 3,478 | 3,171 | 3,629 | 3,308 | 3,476 |
| Tanganyika (Ikola) | 3,482 | 3,175 | 3,633 | 3,312 | 3,480 |
| **Kigoma** | **3,463** | **3,156** | **3,614** | **3,293** | **3,462** |
| Uvinza (Lugufu) | 3,453 | 3,147 | 3,604 | 3,283 | 3,452 |
| Buhigwe | 3,461 | 3,154 | 3,612 | 3,291 | 3,459 |
| Kakonko | 3,463 | 3,156 | 3,614 | 3,293 | 3,461 |
| Kasulu | 3,472 | 3,165 | 3,623 | 3,302 | 3,471 |
| Kibondo | 3,470 | 3,163 | 3,621 | 3,300 | 3,468 |
| **Kilimanjaro (Moshi)** | **3,184** | **3,031** | **3,686** | **3,208** | **3,373** |
| Hai (Bomang'ombe) | 3,187 | 3,035 | 3,689 | 3,211 | 3,376 |
| Mwanga | 3,177 | 3,024 | 3,679 | 3,201 | 3,366 |
| Rombo (Mkuu) | 3,200 | 3,048 | 3,702 | 3,225 | 3,394 |
| Same | 3,170 | 3,018 | 3,672 | 3,194 | 3,359 |
| Siha (Sanya Juu) | 3,190 | 3,038 | 3,692 | 3,215 | 3,380 |
| **Lindi** | **3,275** | **2,992** | **3,666** | **3,178** | **3,358** |
| Lindi-Mtama | 3,279 | 2,997 | 3,671 | 3,183 | 3,376 |
| Kilwa Masoko | 3,299 | 3,016 | 3,690 | 3,202 | 3,333 |
| Liwale | 3,310 | 3,028 | 3,702 | 3,214 | 3,379 |
| Nachingwea | 3,295 | 3,012 | 3,686 | 3,198 | 3,387 |
| Ruangwa | 3,301 | 3,019 | 3,692 | 3,205 | 3,389 |
| **Manyara (Babati)** | **3,228** | **3,076** | **3,730** | **3,253** | **3,422** |
| Hanang (Katesh) | 3,239 | 3,086 | 3,741 | 3,263 | 3,432 |
| Kiteto (Kibaya) | 3,243 | 3,091 | 3,745 | 3,268 | 3,433 |
| Mbulu | 3,241 | 3,088 | 3,743 | 3,265 | 3,434 |
| Simanjiro (Orkasumet) | 3,260 | 3,108 | 3,762 | 3,285 | 3,454 |
| **Mara (Musoma)** | **3,479** | **3,173** | **3,630** | **3,309** | **3,478** |
| Musoma Vijijini (Busekela) | 3,520 | 3,213 | 3,671 | 3,350 | 3,519 |
| Rorya (Ingirijuu) | 3,488 | 3,181 | 3,639 | 3,318 | 3,487 |
| Rorya (Shirati) | 3,523 | 3,216 | 3,674 | 3,353 | 3,522 |
| Bunda | 3,471 | 3,164 | 3,622 | 3,301 | 3,469 |
| Bunda (Kisorya) | 3,480 | 3,173 | 3,631 | 3,310 | 3,479 |
| Butiama | 3,476 | 3,169 | 3,627 | 3,306 | 3,475 |
| Serengeti (Mugumu) | 3,525 | 3,218 | 3,676 | 3,355 | 3,524 |
| Tarime | 3,491 | 3,184 | 3,641 | 3,320 | 3,489 |
| Tarime (Kewanja/Nyamongo) | 3,495 | 3,188 | 3,646 | 3,325 | 3,494 |
| **Mbeya** | **3,408** | **3,101** | **3,559** | **3,238** | **3,406** |
| Chunya | 3,417 | 3,111 | 3,568 | 3,247 | 3,416 |
| Chunya (Makongolosi) | 3,423 | 3,116 | 3,574 | 3,253 | 3,421 |
| Chunya (Lupa Tingatinga) | 3,425 | 3,118 | 3,576 | 3,255 | 3,423 |
| Kyela | 3,424 | 3,117 | 3,575 | 3,254 | 3,422 |
| Mbarali (Rujewa) | 3,392 | 3,085 | 3,543 | 3,222 | 3,390 |
| Rujewa (Madibira) | 3,405 | 3,098 | 3,556 | 3,235 | 3,404 |
| Rujewa (Kapunga) | 3,402 | 3,095 | 3,553 | 3,232 | 3,400 |
| Rungwe (Tukuyu) | 3,417 | 3,110 | 3,568 | 3,247 | 3,415 |
| **Morogoro** | **3,326** | **3,019** | **3,477** | **3,156** | **3,324** |
| Mikumi | 3,341 | 3,035 | 3,492 | 3,171 | 3,340 |
| Kilombero (Ifakara) | 3,364 | 3,057 | 3,515 | 3,194 | 3,362 |
| Kilombero (Mlimba) | 3,386 | 3,079 | 3,537 | 3,216 | 3,385 |
| Kilombero (Mngeta) | 3,375 | 3,068 | 3,526 | 3,205 | 3,374 |
| Ulanga (Mahenge) | 3,374 | 3,067 | 3,525 | 3,204 | 3,373 |
| Malinyi | 3,385 | 3,078 | 3,536 | 3,215 | 3,383 |
| Kilosa | 3,344 | 3,037 | 3,495 | 3,174 | 3,343 |
| Gairo | 3,344 | 3,037 | 3,495 | 3,174 | 3,343 |
| Mvomero (Wami Sokoine) | 3,336 | 3,029 | 3,487 | 3,166 | 3,335 |
| Mvomero (Sanga Sanga) | 3,326 | 3,019 | 3,477 | 3,156 | 3,324 |
| Turian | 3,351 | 3,044 | 3,502 | 3,181 | 3,349 |
| **Mtwara** | **3,262** | **2,979** | **3,652** | **3,165** | **3,372** |
| Nanyumbu (Mangaka) | 3,298 | 3,015 | 3,689 | 3,201 | 3,421 |
| Masasi | 3,278 | 2,995 | 3,668 | 3,181 | 3,397 |
| Newala | 3,283 | 3,000 | 3,673 | 3,186 | 3,404 |
| Tandahimba | 3,276 | 2,993 | 3,666 | 3,179 | 3,397 |
| Nanyamba | 3,276 | 2,993 | 3,666 | 3,179 | 3,397 |
| **Mwanza** | **3,451** | **3,144** | **3,602** | **3,281** | **3,449** |
| Kwimba | 3,469 | 3,162 | 3,620 | 3,299 | 3,467 |
| Magu | 3,459 | 3,152 | 3,610 | 3,289 | 3,458 |
| Misungwi | 3,445 | 3,138 | 3,596 | 3,275 | 3,444 |
| Sengerema | 3,483 | 3,177 | 3,634 | 3,313 | 3,482 |
| Ukerewe | 3,511 | 3,204 | 3,661 | 3,340 | 3,509 |
| **Njombe** | **3,393** | **3,086** | **3,544** | **3,223** | **3,392** |
| Njombe (Kidegembye) | 3,414 | 3,107 | 3,565 | 3,244 | 3,412 |
| Ludewa | 3,431 | 3,124 | 3,582 | 3,261 | 3,430 |
| Makambako | 3,386 | 3,079 | 3,536 | 3,216 | 3,384 |
| Makete | 3,424 | 3,117 | 3,575 | 3,254 | 3,423 |
| Wanging'ombe (Igwachanya) | 3,391 | 3,084 | 3,542 | 3,221 | 3,389 |
| **Rukwa (Sumbawanga)** | **3,474** | **3,167** | **3,625** | **3,304** | **3,472** |
| Sumbawanga Rural (Mtowisa) | 3,474 | 3,167 | 3,625 | 3,304 | 3,472 |
| Kalambo (Matai) | 3,481 | 3,174 | 3,632 | 3,311 | 3,479 |
| Nkasi (Namanyele) | 3,487 | 3,180 | 3,638 | 3,317 | 3,486 |
| **Ruvuma (Songea)** | **3,347** | **3,064** | **3,738** | **3,250** | **3,423** |
| Mbinga | 3,360 | 3,077 | 3,751 | 3,263 | 3,435 |
| Namtumbo | 3,338 | 3,055 | 3,729 | 3,241 | 3,428 |
| Nyasa (Mbamba Bay) | 3,385 | 3,102 | 3,776 | 3,288 | 3,446 |
| Tunduru | 3,313 | 3,030 | 3,703 | 3,216 | 3,402 |
| **Shinyanga** | **3,430** | **3,123** | **3,581** | **3,260** | **3,429** |
| Kahama | 3,443 | 3,137 | 3,594 | 3,273 | 3,442 |
| Kishapu | 3,458 | 3,151 | 3,609 | 3,288 | 3,457 |
| Ushetu (Nyamilangano) | 3,461 | 3,154 | 3,612 | 3,291 | 3,459 |
| Ushetu (Kangeme Village) | 3,452 | 3,145 | 3,603 | 3,282 | 3,450 |
| Salawe | 3,444 | 3,138 | 3,595 | 3,274 | 3,443 |
| **Simiyu (Bariadi)** | **3,471** | **3,164** | **3,622** | **3,301** | **3,470** |
| Busega (Nyashimo) | 3,464 | 3,157 | 3,615 | 3,294 | 3,463 |
| Itilima (Lagangabilili) | 3,474 | 3,167 | 3,625 | 3,304 | 3,473 |
| Maswa | 3,463 | 3,156 | 3,614 | 3,293 | 3,461 |
| Meatu (Mwanhuzi) | 3,470 | 3,163 | 3,621 | 3,300 | 3,468 |
| **Singida** | **3,392** | **3,085** | **3,542** | **3,222** | **3,390** |
| Iramba | 3,404 | 3,097 | 3,555 | 3,234 | 3,402 |
| Manyoni | 3,376 | 3,069 | 3,527 | 3,206 | 3,375 |
| Itigi (Mitundu) | 3,392 | 3,085 | 3,543 | 3,222 | 3,390 |
| Ikungi | 3,387 | 3,080 | 3,538 | 3,217 | 3,385 |
| Mkalama (Nduguti) | 3,416 | 3,109 | 3,567 | 3,246 | 3,415 |
| **Songwe (Vwawa)** | **3,417** | **3,110** | **3,568** | **3,247** | **3,416** |
| Songwe (Mkwajuni) | 3,424 | 3,117 | 3,575 | 3,254 | 3,423 |
| Ileje | 3,421 | 3,114 | 3,572 | 3,251 | 3,420 |
| Momba (Chitete) | 3,426 | 3,119 | 3,577 | 3,256 | 3,425 |
| Tunduma | 3,421 | 3,114 | 3,572 | 3,251 | 3,420 |
| **Tabora** | **3,409** | **3,102** | **3,560** | **3,239** | **3,408** |
| Igunga | 3,409 | 3,102 | 3,560 | 3,239 | 3,407 |
| Kaliua | 3,422 | 3,115 | 3,573 | 3,252 | 3,421 |
| Ulyankulu | 3,419 | 3,113 | 3,570 | 3,249 | 3,418 |
| Nzega | 3,419 | 3,113 | 3,570 | 3,249 | 3,418 |
| Sikonge | 3,418 | 3,111 | 3,569 | 3,248 | 3,416 |
| Urambo | 3,419 | 3,112 | 3,570 | 3,249 | 3,417 |
| Uyui | 3,415 | 3,108 | 3,566 | 3,245 | 3,414 |
| Mpyagula | 3,441 | 3,134 | 3,592 | 3,271 | 3,439 |
| **Tanga** | **3,137** | **2,985** | **3,639** | **3,162** | **3,345** |
| Handeni | 3,158 | 3,006 | 3,660 | 3,182 | 3,325 |
| Kilindi | 3,173 | 3,021 | 3,675 | 3,197 | 3,359 |
| Korogwe | 3,150 | 2,997 | 3,651 | 3,174 | 3,338 |
| Lushoto | 3,159 | 3,006 | 3,661 | 3,183 | 3,348 |
| Mkinga (Maramba) | 3,144 | 2,992 | 3,646 | 3,169 | 3,360 |
| Muheza | 3,142 | 2,990 | 3,644 | 3,167 | 3,345 |
| Pangani | 3,144 | 2,992 | 3,646 | 3,169 | 3,352 |

## JEDWALI B: BEI ZA JUMLA (Shs/Lita)

| Bandari | Bei za Petroli bila ruzuku | Bei za Petroli baada ya ruzuku | Bei ya Dizeli bila ruzuku | Bei ya Dizeli baada ya ruzuku | Mafuta ya Taa |
|---|---|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 3,168.59 | 2,862.59 | 3,318.70 | 2,998.70 | 3,167.28 |
| Tanga | 3,005.73 | 2,853.73 | 3,505.72 | 3,029.72 | 0 |
| Mtwara | 3,129.51 | 2,847.51 | 3,518.69 | 3,032.69 | 0 |

Mha. Modestus M. Lumato

**MKURUGENZI MKUU- EWURA**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mwongozo madini kimkakati muhimu kwa taifa

**TANZANIA** imebarikiwa kuwa na rasilimali nyingi chini ya ardhi ikiwamo madini ya kimkakati (critical mining), ambayo yanahitajika duniani kwa ajili ya kutengeneza bidhaa mbalimbali.

Utafiti umebaini kuwapo aina 17 za madini ya kimkakati ambayo yanatakiwa sana duniani, hasa kwa ajili ya kuzalisha nishati jadidifu, iliyoonekana rafiki wa mazingira kuliko nishati ya mafuta, gesi na makaa ya mawe.

Nchi zilizogundua baadhi ya madini zimeweka mwongozo na sera ambazo zimeweka tafsiri ya rasilimali hiyo na mtu yeyote haruhusiwi kuitumia au kuchimba bila kulinda maslahi ya nchi husika.

Hadi sasa nchi zenye sera maalum kwa ajili ya madini ya kimkakati ni Marekani, Asia na Ulaya, ambazo kila mmoja ameitafsiri kwa kadri inavyoona ni muhimu kwa nchi na watu wake na kuzilinda.

Mathalani, kwa Afrika madini ya cobalt ambayo ni asilimia 70 ya malighafi ya kutengeneza betri aina zote dunia, yanapatikana nchini Congo. Kwa mujibu wa mtaalamu wa madini na mjiolojia, Bosco Tindyebwa, rasilimali hiyo adimu inapatikana maeneo ya Kabanga, Tanzania baadhi ya madini ya kimkakati yanapatikana eneo la Kabanga, Pandahill, Ngualla, Wingu na Mahenge.

Alisema kama dunia inakubali kuwa madini ya cobalt yanapatikana kwa wingi Congo, maana yake itaendelea kuitegemea nchi hiyo kwa malighafi, lakini swali la kujiuliza kuna sera na sheria za kuilinda, watanambua umuhimu wake na kwa kiasi gani wananchi wananufaika, pia msimamo wa Afrika ukoje.

Alitoa mfano kuwa nchi za kiarabu zimeendelea kwasababu zimeshikilia vyema rasilimali ya mafuta, na uhusiano wao na Marekani ni kwenye bidhaa hiyo kwa kuwa wameweka msimamo kuwa kama unataka mafuta yetu msimamo ni huo na umeheshimika.

Lakini ni lazima serikali ije na mkakati ya kulinda na kutumia madini ya kimkakati hasa katika kipindi cha mpito cha mabadiliko ya nishati duniani.

Pia ni muhimu nchi kutambua siasa za dunia na kuweka mwongozo wa kulinda rasilimali hizo, lakini kuangalia namna salama ya kuhama kutoka kwenye nishati ya mafuta, gesi na makaa ya mawe kwenda kwenye nishati jadidifu ambayo ni jua, upepo, mawimbi ya bahari, upepo wa baharini na kinyesi cha ng'ombe.

Gesi asilia na mafuta viligundulika kwa mara ya kwanza nchini mwaka 1974 katika kisiwa cha Songosongo mkoani Lindi, ukafuatiwa na ugunduzi mwingine mwaka 1982 eneo la Mnazibay na kufanya jumla ya kiasi cha nishati hiyo iliyogundulika nchi kavu na baharini kuwa takribani futi za ujazo trilioni 55.08 hadi Machi 2015.

Wananchi wa mikoa hiyo walikuwa na matumaini makubwa kwa kuwa waliaminishwa mikoa yao itakuwa na maendeleo makubwa kiasi cha kufananishwa na Dubai, huku wakizuia isitoke hadi vikatumika vyombo vya dola kuwatuliza.

Juzi Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Felchesmi Mramba, katika kipindi maalum cha mafanikio ya sekta ya nishati alieleza mpango wa kujenga vituo vikubwa vinne na vidogo vya kuuza gesi ya magari jijini Dar es Salaam, huku kampuni 18 zikionyesha nia ya kuwekeza eneo hilo. Jitihada hizi zinafanyika wakati ambao dunia imeshaanza kuhakama taratibu kwenda kwenye nishati jadidifu, huku taasisi za fedha kama Benki ya Dunia (WB) na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na nyingine, zikipunguza mikopo kwenda nishati hiyo.

Katika mkutano COP26 (Conference of Parties 26), kila nchi ilitakiwa kuweka mpango wa kupunguza hewa ukaa ifikapo 2030 na 2050, kwa kuondokana na matumizi ya nishati za gesi, mafuta na makaa ya mawe na zaidi kujikita kwenye nishati jadidifu.

Ni lazima Tanzania iwe makini katika uhamaji wa nishati hizo, wasijitokeze wawekezaji wakataka kuwekeza kwa muundo ambao Watanzania hawatapata faida na kwa kuwa tupo kipindi cha mpito iwe ni vigumu kuwakatalia.

Pia, lazima kujua wanapochukua hiyo rasilimali yetu wanaitumia au ni kwa ajili ya kwenda kuhifadhi ili inapoisha kwenye chanzo watumie, mambo hayo yamefanywa na nchi zilizoendelea na haitashangaza yakifanyika sasa, ndiyo maana tunasema lazima kuja na msimamo wa matumizi ya madini ya kimkakati.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Muungwana Lazima Nilonge

# Kama sigara inaua nusu ya wanaoivuta unaihitaji?

Na Sabato Kasika

**MEI** 31, hapo jana kilikuwa kilele cha maadhimisho ya kupinga matumizi ya tumbaku duniani.

Ukiangalia hali ilivyo nchini,unaweza kudhani watu wanasikia lakini ujumbe unaingia sikio la kulia, unatokea sikio la kushoto, hakuna anayeona kuwa tumbaku ni kitisho.

Ikimaanisha hakuna, kujali wala kutilia maanani. Ni kawaida kuwakuta watu wanavuta sokoni, stendi za daladala, barabarani, shuleni na maeneo yenye mikusanyiko mikubwa.

Katika mazingira hayo, hata wale wasiovuta, wanakula moshi wa sigara bila ridhaa yao na kuwa kwenye hatari ya kupata maradhi yanayosababishwa na uvutaji wa tumbaku.

Wakati huu wa kilele inashangaza kuona kuwa jamii inazidi kupofuka kuhusu athari za tumbaku.

Moja ya malengo ya maadhimisho haya ni kuifanya jamii kutambua madhara ya tumbaku na kuwa makini na uvutaji wake ambao unachangia ongezeko la saratani na magonjwa sugu.

Hata hivyo, pamoja na juhudi hizo za kutaka kuinusuru jamii dhidi ya uvutaji au uvutishwaji wa tumbaku, inaonekana baadhi ya watu hawajaelewa umuhimu wake.

Hilo linatokana na ukweli kwamba, licha ya kuwapo kwa maelekezo ya kutovuta sigara kwenye mkusanyiko wa watu, uvutaji unazidi kuwa endelevu.

Juhudi zaidi zinahitajika kuelimisha umma tena kwa kuwafikia watu kwenye mikusanyiko na kuwaelezea madhara ya kutumia tumbaku ili waachane nayo.

Jitihada za Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), za kulinda afya za Watanzania, ikiwakumbusha kuwa uvutaji wa tumbaku kwenye maeneo yanayotumiwa na watu wengi hairuhusiwi zinafanyika lakini hazizingatiwi ipasavyo.

Kifungu cha Sheria ya Udhibiti wa Bidhaa za Tumbaku, sura 121 kimetafsiri maeneo ya umma kama mahali ambapo inatolewa huduma ya afya, maktaba, mahali pa ibada, majengo au maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya mikutano ya kitamaduni na kijamii.

Kwingineko ni katika shughuli za michezo au burudani, sehemu za huduma ya chakula, ofisi, vyombo vya usafiri wa aina zote, mabanda ya maonyesho, masoko na maduka makubwa.

TMDA inasema, katika sehemu za umma sheria inakataza uvutaji wa aina yoyote wa bidhaa za tumbaku na kuelekeza bango lenye maneno yanayosomeka,"hairuhusiwi kuvuta sigara".

Aidha, TMDA inafafanua kuwa, kifungu cha 13 cha Sheria ya Udhibiti wa Bidhaa za Tumbaku, kimeruhusu uvutaji kwenye baadhi ya maeneo ikiwa ni pamoja na taasisi za elimu ya juu, majengo ya ofisi, hoteli, baa, migahawa na maeneo ya burudani ambayo yanapaswa kutenganisha vyumba au maeneo maalum ya kuvutia na kutovutia tumbaku.

Aidha, katika ufafanuzi wake, mamlaka hiyo inasema, kanuni ndogo ya 7 (1) na (2) ya Kanuni za Bidhaa za Tumbaku za mwaka 2014, inawataka wamiliki wa majengo yanayotumiwa na watu wengi kuweka vifaa vya kubaini moshi wa tumbaku na kuweka alama zinazosomeka, 'jengo hili limefungwa mtambo wa kubaini moshi wa tumbaku'.

Hivyo, TMDA inawaagiza wamiliki, wapangaji na waendesha biashara ya majengo yanayotumiwa na watu wengi kuzingatia masharti yasheria na kanuni ilizoanisha.

Pamoja na hatua hizo, wapo baadhi ya wazazi na walezi ambao huwavutisha watoto wao moshi wa sigara, nao ingefaa waelimishwe.

Ni jambo la kawaida kuwapakata watoto huku wakivuta sigara au kuwa ndani ya magari yao huku wakivuta bila kutambua kuwa wanawaumiza.

Kwa hali hiyo, ni wazi kwamba elimu zaidi inahitajika kwa umma kuongeza uelewa wa madhara ya tumbaku.

Ni muhimu wauza sigara kutambua kuwa kila anayeuza naye ni mtumiaji, hata jirani yake naye anavutishwa pia.

Ukweli huo unatokana na mazoea ya kuuza sigara kwani kwa kila anayeziuza awe kwenye vituo vya mabasi, barabarani au dukani lazima awe na kibiriti, kwa ajili ya wateja wao wanaowahudumia na kuwarudishia wauzaji, watoto wao na walio karibu na muuzaji.

Uraibu huo sasa udhibitiwe usiumize wengine, hivyo suala la kutenga maeneo ya kuvutia tumbaku linahitaji kupewa Msukumo mpya.

Shirika la Afya Dunia (WHO) linataja mambo hatari kuhusu kuvuta tumbaku kuwa ni pamoja na kuua nusu ya watumiaji wake, hivi una haja nayo?

# Serikali sasa kuchunguza kilichomo kwenye shisha

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) imeagizwa kufanya tathmini ndani ya miezi miwili ili kujua bidhaa zinazosadikiwa huchanganywa katika shisha.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alitoa agizo hilo jana alipotoa tamko la waziri la maadhimisho ya Siku ya Kutotumia Tumbaku Duniani kwa vyombo vya habari jijini hapa.

"Zipo taarifa lakini hatujathibitisha kwamba shisha inachanganywa na baadhi ya bidhaa zinazosemekana ni dawa za kulevya... shisha nzuri kumbe kuna mambo zaidi ya mengine.

"Kwa hiyo, nimesema badala ya kuanza kukurupuka, kukimbizana na watu wanaofanya shughuli au sehemu za starehe zinazofanya shughuli hii ya shisha, acha niwe na uthibitisho na utafiti wa kisayansi. Je, hiyo shisha ambayo watu wanatumia inawekwa vitu gani?" Ummy alisisitiza.

Hata hivyo, alitoa angalizo kuwa sheria ipo, haijafutwa na kuwataka kukumbuka kuwa biashara ya shisha ni kosa la jinai kwa mujibu wa sheria za nchi. "Nimewataka TMDA ndani ya miezi miwili, ninajua kuna utafiti ule mwingine wa kimaabara, tupeni miezi miwili hata tukipata sampuli 50 tupeleke maabara ili kujua shisha ina vitu gani, na endapo tutabaini kuna dawa za kulevya, itakuwa ni sababu kubwa ya kumwomba Waziri Mkuu kupitia Mamlaka ya Kupamba na Dawa za Kulevya kuungana na sisi kupinga matumizi ya shisha.

"Sisi tunapinga kuna madhara kwa binadamu, hivyo kwenye hili tusikurupuke tuwe na tathmini za kisayansi ili kujua zinawekwa kitu gani, kama ni sigara ya kawaida, kazi yetu ni kuhamasisha watu wasivute sigara," alisema.

Ummy alisema katika kudhibiti matumizi ya tumbaku nchini, wameunda Kamati ya Taifa ya Udhibiti wa Bidhaa za Tumbaku ambayo ina wawakilishi kutoka wizara yake na idara mbalimbali, ikiwa na jukumu la kutoa ushauri katika masuala mbalimbali ya udhibiti wa bidhaa hiyo nchini.

"Ninawahakikishia Watanzania ndani ya wiki mbili ukiacha kuvuta tumbaku, uwezo wa mapafu unaongezeka, ndani ya wiki kama unavuta sigara au tumbaku, ndani ya miaka 10 hatari ya kupata saratani kwenye mapafu inapungua kwa asilimia 50," alisema.

Pia alisema mwaka huu utafanyika utafiti wa kitaifa kuhusu visababishi vya magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Kaimu Meneja wa TMDA kanda ya kati, Seraphina Cleophace, alisema bado hawajawa na utafiti ambao umebaini vitu ambavyo vinachanganywa katika shisha.

Mkurugenzi Msaidizi wa Magonjwa Yasiyoambukiza wa Wizara hiyo, Dk. James Kapologwe, alisema takwimu zinaonyesha asilimia 8.7 ya Watanzania, sawa na watu milioni 2.6, wanavuta tumbaku.

"Pia asilimia 77 ya moshi wa tumbaku unapatikana katika baa, migahawa asilimia 31 huku majumbani ikiwa ni asilimia 13.8," alisema.




Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), Dk. Edwin Mhede (kushoto), akiwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, Abdalah Chaurembo, kwenye basi la mwendokasi, walipokua kwenye ziara ya kikazi kwenye miundombinu ya DART, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# ZAECA yashikilia wahasibu 2 tuhuma za ubadhirifu bil. 1.3/-

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA), inawashikilia wahasibu wawili kwa tuhuma za ubadhirifu wa fedha Sh. bilioni 1.3 wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Ahmed Makarani aliwataja wahasibu hao kuwa ni Mohammed Mussa Usi (53) na Issa Barak Abdallah (42).

Alisema watuhumiwa hao walijipatia fedha hizo baada ya kuanzisha miradi hewa ikiwamo ya ujenzi na ukarabati wa barabara.

"Kuna makosa matatu tunayafanyia uchunguzi yakiwemo ya rushwa, uhujumu uchumi na ubadhilifu wa fedha za umma," alisema Makarani. Alisema wahasibu hao walifanya vitendo vya udanganyifu kwa kuanzisha kampuni hewa na miradi hewa na kufanikiwa kuchukua kiwango hicho cha fedha kinyume na sheria.

"Mwaka huu kwa nyakati tofauti bila uhalali wahasibu hao walijipatia fedha Shilingi bilioni moja na milioni mia tatu baada ya kudanganya kampuni na miradi hewa," alisema.

Alisema ZAECA imeamua kukamata mali za watuhumiwa hao, ikiwamo magari manane, mashamba matano, nyumba tatu na Dola za Kimarekani 50,000.

Alisema, uchunguzi unaonesha watuhumiwa walikuwa wakifanya vitendo vya utakatishaji fedha jambo ambalo ni kinyume na Sheria na Upelelezi unaendelea kufanyika kwa haraka kabla jalada la uchunguzi kuwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar.

Alifafanua kuwa ZAECA imebaini miradi iliyokuwa ikitumia fedha za umma haipo na wala kampuni hazipo pamoja na kutumika malipo ya karibu Sh. bilioni 1.3 fedha za serikali.

## Wataka mwendokasi kutumika Sabasaba

**Na Joseph Mwendapole**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, imeagiza Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka (DART), kuhakikisha wananchi wanapata usafiri wa mabasi ya mwendokasi kipindi cha maonyesho ya kimataifa ya biashara ya Sabasaba.

Agizo hilo lilitolewa juzi jijini Dar es Salaam na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Abdalah Chaurembo, wakati wa majumuisho ya ziara ya kutembelea DART kujionea inavyotekeleza majukumu yake.

"Kwa kuwa miundombinu haijakamilika kwa asilimia mia moja ni vyema DART mkaangalia Sabasaba ya mwaka huu, wananchi waletwe huku kwa mabasi yenu, hii itapunguza kero ya usafiri, lakini itaamsha ari ya wana Mbagala ambao wanasubiri usafiri huu kwa hamu kubwa baada ya mradi kukamilika," alisema Chaurembo.

Vile vile, alisema Rais Samia Suluhu Hassan ana matumaini makubwa mradi utakamilika kwa wakati na kuanza kazi kabla ya Machi mwakani, na kwamba DART iendelee kusimamia ukamilishaji wa mradi huo, ili wananchi wa Mbagala waondokane na adha ya usafiri wa umma iliyowakabili kwa muda mrefu.

Agizo lingine la kamati hiyo ni pamoja na DART kuandaa utaratibu ambao kamati itauridhia kwa ajili ya kulishauri Bunge namna bora ya kudhibiti mwingiliano mkubwa wa magari yanayopita katika barabara maalum za mabasi hayo.

Chaurembo alimtaka mtoa huduma katika barabara hizo, kampuni ya UDART kuwasilisha kwa kamati taarifa ya changamoto zilizopo za uchache na ubovu wa mabasi na Wakala pia umsimamie kwa karibu zaidi mkandarasi anayesimamia ujenzi wa barabara hizo ambaye ni Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS).

Pia, aliutaka Wakala kuangalia namna utakavyodhibiti bodaboda ambazo zimekuwa zikisababisha ajali katika mfumo wa njia za DART.

Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu wa DART, Dk. Edwin Mhede, alisema wakala umeyapokea maagizo ya kamati na utayafanyia kazi, ili kuboresha usafiri wa umma katika Jiji la Dar es Salaam na maeneo ya jirani.

"Mwenyekiti niwahakikishie kwamba maagizo yote mliyotoa tutayafanyia kazi kwa wakati na tunaishukuru sana kamati yako kwa kutembelea mradi na kuona maendeleo yake," alisema Dk. Mhede.

Ziara ya kamati hiyo ilihudhuriwa pia na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI), David Silinde, Wajumbe wa Kamati, Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam na Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI, Dk. Charles Msonde.

Wengine ni Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Heri James, Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo, pamoja na wakuu wa taasisi zinazohusika na masuala ya usafirishaji.

# IUCEA yapongezwa ufadhili masomo

**Na Mwandishi Wetu**

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimeungana na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Dk Peter Mathuki, kulipongeza Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki (IUCEA) kwa kutekeleza Mpango wa Ufadhili wa Masomo kwa wanafunzi kutoka nchi wanachama wa jumuiya hiyo unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (Kfw).

Mpango huo wa ufadhili wa masomo unaojulikana kama EAC KfW ni sehemu ya programu tano za ufadhili zinazosimamiwa na IUCEA kama sehemu ya utekelezaji wa elimu ya juu katika ukanda wa Afrika Mashariki.

"Chuo cha Taifa cha Usafirishaji kinapenda kulipongeza Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki (IUCEA) kwa utekelezaji wa mpango wa ufadhili huu wa masomo kwa wanafunzi," Ofisa Uhusiano wa NIT, Ngusekela David, alisema katika warsha elekezi kwa wanafunzi wanaonufaika na program hiyo ya ufadhili wa masomo uliofanyika jijini Dar es Salaam.

David alisema NIT iko katika hatua nzuri za kujiunga na IUCEA ili kupata manufaa ya ushirikiano kutoka kwa vyuo vikuu wanachama vya ukanda huo.

"Kwa sasa tuko kwenye mchakato wa kuwakilisha nyaraka zetu IUCEA ili kusajiliwa kama mwanachama mpya wa baraza hilo," alisema David.

Aliongezea kuwa baada ya kujiunga na baraza hilo, NIC itapata faida nyingi zinazotolewa na IUCEA kwa vyuo vikuu washirika katika ukanda wa Afrika Mashariki.

"Chuo chetu cha NIT hakitaki kupoteza fursa nzuri ambazo hutolewa na IUCEA kwa wanachama wao. Tunaahidi kuhitimisha haraka iwezekanavyo mchakato wote ili tuweze kusajiliwa kama mwanachama mpya wa baraza hilo," alisema.

Akizungumza wakati akifungua warsha elekezi hiyo, Dk Mathuki aliipongeza IUCEA kwa kusimamia mpango huo wa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi.

Alisema kuwa mpango huo kutoka EAC kwa sekretarieti yake EAC, ni njia mojawapo ya kuandaa wataalamu na viongozi wazuri katika jumuiya yetu.

"Lengo la ufadhili huu ni kutoa mafunzo kwa vijana kutoka katika jumuiya yetu ambao watakuja kuwa viongozi ambao watakuza ushirikiano mzuri kwa nchi zetu za ukanda wa Afrika Mashariki," alisema.

"Tunaamini kuwa vijana hawa ambao wanapata ufadhili huu watakuwa mawakala wazuri wa mabadiliko chanya ya baadaye katika eneo letu hili, ambao watadumisha ajenda ya ushirikiano kwa nchi zetu," aliongeza.

Alitanabaisha kuwa vijana hao ambao wanapatiwa ufadhili wa masomo watakuwa tayari kuleta mabadiliko ya kiuchumi na maendeleo katika nchi zetu za Afrika ya Mashariki.

Katibu Mtendaji wa IUCE, Prof. Gaspard Banyankimbona, aliwapongeza washindi wote wa kundi la pili la mpango wa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi kutoka Afrika Mashariki.

Alisema mpango huo wa ufadhili wa masomo ulianza mwaka 2018 wakati wanufaika wakuu wakiwa vijana wote wanafunzi kutoka nchi zote za EAC ukifadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (Kfw).




Makamu wakuu wa vyuo vikuu vya Afrika Mashariki (EAC), wakijadiliana jambo wakati wa semina elekezi kwa wanafunzi wanufaika wa Mpango wa Ufadhili wa Masomo kwa wanafunzi kutoka nchi zote za EAC unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (Kfw), jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Kilichombeba Mwijaku kuachiwa huru kortini

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imemwachia huru msanii wa maigizo, Bulton Mwemba, maarufu Mwijaku, aliyekuwa anakabiliwa na mashtaka ya kusambaza picha za utupu mtandaoni baada ya upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha kosa.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rhoda Ngimilanga, baada ya upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha kesi hiyo bila kuacha shaka yoyote.

Hakimu Ngimilanga alisema upande wa mashtaka ndiyo wenye mamlaka ya kuthibitisha kesi, hivyo anamwachia mshtakiwa Mwijaku kwa sababu wameshindwa kuthibitisha kosa lake.

Hakimu Ngimilanga pia alisema katika ripoti ya upande wa mashtaka, haioneshi kama simu ya Mwijaku ndiyo ilisambaza picha za utupu.

Mwijaku alikuwa anakabiliwa na kesi ya kusambaza picha za utupu kinyume cha sheria na alijitetea akiwa na mashahidi wake wawili.

Mei 2, mwaka huu, Mwijaku alipatikana na kesi ya kujibu wakati kesi hiyo ilipoletwa kwa ajili ya kutolewa uamuzi kama ana kesi ya kujibu au la, baada ya upande wa mashtaka kumaliza kutoa ushahidi.

Baada ya kutolewa uamizi huo, Mwijaku alidai mahakamani kwamba angekuwa na mashahidi watatu wakati wa kutoa utetezi wake.

Wakati wa usikilizwaji wa kesi hiyo, upande wa mashtaka ulikuwa na mashahidi watano pamoja na vielelezo vinne.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo katika tarehe tofauti kati ya Septemba 17 hadi Oktoba 10 mwaka 2019 jijini Da r es Salaam.

Ilidaiwa kuwa katika tarehe hizo, alisambaza picha za utupu akitumia kompyuta yake kupitia mtandao wa WhatsApp.

# TBL yazindua mfumo malipo kwa wakulima

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Tanzania Breweries Limited (TBL), ikishirikiana na Vodacom Tanzania, imetangaza rasmi kuunganisha huduma za malipo ya wakulima wake na mtandao wa BanQu ili kuongeza ufanisi na uwazi kwenye malipo ya wakulima pamoja na kuwawezesha kiuchumi.

BanQu ni mfumo wa programu ambao umekuwa ukitoa huduma ya kuhifadhi data na kutunza kumbukumbu za wagavi (wakulima) wanaouza malighafi kwa kampuni mama za TBL iitwayo AB InBev.

Kwenye matumizi ya huduma hiyo, Vodacom Tanzania imeungana na TBL ambapo huduma ya ununuzi na malipo imeunganishwa na M-Pesa, hivyo malipo yanaweza kufanyika moja kwa moja. Mkurugenzi Mtendaji wa TBL, Jose Moran alisema jana jijini Dar es Salaam kuwa mpaka sasa tayari wakulima 6,500 wanaoza mazao yao kwa TBL, wameshaungwanishwa kwenye mfumo wa programu ya BanQu .

Wakulima hao ni pamoja na wa zabibu, mtama na shayiri ambao waliunganishwa mwezi Desemba mwaka jana kama sehemu ya jaribio la matumizi ya mfumo wa BanQu. Matumizi ya mfumo huu hayana ulazima wa matumizi ya simu janja, hivyo hata wakulima wenye simu za kawaida wanaweza kuutumia mfumo huu kupitia huduma ya ujumbe mfupi, hivyo wakulima wengi zaidi wanaweza kufikiwa.

Alisema teknolojia hiyo imejikita kupunguza ubadhirifu kwenye malipo ya wakulima, hivyo kuwawezesha wakulima kiuchumi na kuwaongezea wigo wa kupata mikopo na huduma zingine za kifedha.

Akizungumza kwenye uzinduzi, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia, Nape Nnauye, alisema: "Mfumo wa BanQu uliolenga kuwaongezea uwezo wakulima, umekuja wakati mwafaka kwani unaenda sambamba na kampeni maalum ya kukuza kilimo ya 'Ajenda 10/30' iliyozinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan hivi karibuni.

"Hatua hii inathibitisha kuwa TBL inakwenda sambamba na ajenda ya serikali ya kuleta maendeleo kwa kutumia teknolojia na ubunifu na hatimaye kuwawezesha wakulima kiuchumi. Ninawapongeza TBL na Vodacom kwa kushirikiana kuletea wakulima suluhisho la kivumbuzi kwa kutumia teknolojia."

Mkurugenzi Mtendaji wa TBL, Jose Moran alisema: "Kupitia teknolojia ya BanQu, sasa tunaweza kuhakikisha kuwa wakulima wetu wana uwezo wa kupata suluhisho na taarifa zitakazo wawezesha kufanya uamuzi sahihi.

"Mfumo wa programu ya BanQu imetengenezwa ili kuwalinda wakulima, kuwaongezea fursa za kupata huduma za kifedha kupitia washirika wetu Vodacom Tanzania, na kwa namna hii tutaongeza uwazi na hatimaye kukuza ukuaji wa uchumi jumuishi."

Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania, Sitholizwe Mdlalose, alipongeza ushirikiano huo na kusema kuwa tangu kuanzishwa kwa M-Pesa mwaka 2008, huduma hiyo imechangia kwa kiasi kikubwa kwenye kupanua wigo wa huduma za kifedha na huduma za malipo ya kidigitali Tanzania.

Hivi sasa asilimia 74 ya malighafi inayotumiwa na TBL inatoka kwa wakulima wa ndani ya nchi. TBL imeweka mkakati wa kuhakikisha kuwa asilimia 100 ya wakulima wake wanapatiwa ujuzi, wanaunganishwa na huduma za kifedha na kuwezeshwa kiuchumi kufikia mwaka 2025, mwaka ambao ni ukomo wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Juni 1999 hadi 2025.

# Wahitimu kidato VI waitwa wafunzo JKT

Na Gwamaka Alipipi

JESHI la Kujenga Taifa (JKT) limewataka wahitimu wa kidato cha sita mwaka 2022 kutoka shule zote Tanzania Bara kuhudhuria mafunzo kwa mujibu wa sheria katika kambi walizopangiwa kuanzia Juni 3 hadi 17, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Tawi la Utawala JKT, Brigedia Jenerali Hassan Mabena, alisema kwa wahitimu wenye ulemavu wa kuonekana kwa macho wanatakiwa kuripoti katika Kambi ya Ruvu JKT iliyoko Mlandizi mkoani Pwani, ambayo ina miundombinu ya kuhudumia watu wa jamii hiyo.

Brigedia Jenerali Mabena alisema: "Jeshi la Kujenga Taifa linawaita vijana waliohitimu elimu ya sekondari kidato cha sita kwa mwaka 2022 kutoka shule zote za Tanzania Bara kuhudhuria mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria."

Alisema vijana walioitwa wamepangiwa katika kambi za JKT Rwamkoma-Mara, JKT Msange-Tabora, JKT Ruvu-Pwani, JKT Mpwapwa na Makutupora JKT-Dodoma.

Alizitaja kambi zingine ni JKT Mafinga-Iringa, JKT Mlale-Ruvuma, JKT Mgambo na JKT Maramba-Tanga, JKT Makuyuni-Arusha, JKT Bulombora, JKT Kanembwa, JKT Mtabila-Kigoma, JKT Itaka-Songwe, JKT Luwa na JKT Milundikwa-Rukwa, JKT Nachingwea-Lindi na JKT Kibiti-Pwani na Oljoro JKT-Arusha.

"JKT inawataka vijana hao kuripoti katika kambi hizo wakiwa na vifaa mbalimbali ikiwamo bukta ya rangi ya bluu nyeusi yenye mpira kiunoni iliyo na mfuko mmoja nyuma, urefu unaoishia magotini, isiyo na zipu, fulana ya kijani, raba za michezo rangi ya kijani au bluu, shuka mbili za kulalia zenye rangi ya bluu bahari," alisema Brigedia Jenerali Mabena.

Aliongeza: "Pia waje na soksi ndefu za rangi nyeusi, nguo za kuzuia baridi kwa waliopangiwa mikoa yenye baridi, traki suti ya rangi ya kijani au bluu, nyaraka zote zinazohitajika katika udahili wa kujiunga na elimu ya juu ikiwamo cheti za kuzaliwa, vyeti vya kuhitimu kidato cha nne, pamoja na nauli ya kwenda kambini na kurudi nyumbani."

Brigedia Jenerali Mabena alisema orodha kamili ya majina ya vijana walioitwa kwenye kambi walizopangiwa na maeneo yaliyopo pamoja na vifaa wanavyotakiwa kwenda navyo inapatikana katika tovuti ya JKT ambayo ni www.jkt.go.tz



Waratibu wa warsha ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) Uwezeshaji Jinsia na Vijana Kiuchumi, (kutoka kushoto walioketi) ni Meneja wa Programu wa masuala ya vyombo vya kifedha kutoka Umoja wa Ulaya nchini Tanzania, Mihaela Marcu, Mkurugenzi wa Mipango, Sera na Utafiti wa TADB, Mzee Kilele, Mshauri wa mifumo ya Kimaendeleo ya Kifedha kutoka ICR, Sarah Weiss na Meneja Uhamasishaji wa Rasilimali kutoka TADB, Emmanuely Lyimo, wakiwa pamoja na washiriki wa warsha hiyo, iliyofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki ya Exim yatoa msaada wa madawati

**Na Mwandishi Wetu,** SHINYANGA

BENKI ya Exim Tanzania imekabidhi msaada wa madawati 100 yenye thamani ya Sh. milioni 20 kwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, ili kuunga mkono jitihada za mkoa huo katika kukabiliana na shida zinazoikabili sekta ya elimu ikiwamo kero ya uhaba wa madawati.

Madawati hayo yatagawanywa kwenye shule zinazokabiliwa zaidi na uhaba wa madawati mkoani hapo.

Akizungumza kwenye hafla fupi ya kukabidhi madawati hayo iliyofanyika kwenye ofisi ya Mkuu wa Mkoa mjini hapa mwishoni mwa wiki, Mkuu wa Matawi ya Benki ya Exim, Agnes Kaganda, alisema ni mwendelezo wa mkakati wa benki hiyo unaofahamika kama Exim Cares unaolenga kugawa madawati zaidi ya 1,000 katika mikoa mbalimbali nchini na ni sehemu tu jitihada ambazo benki hiyo imekuwa ikifanya kusaidia jamii inayoizunguka. Alisema kuwa benki hiyo imekuwa mstari wa mbele kushirikiana na serikali katika kufanikisha mipango mbalimbali husu-sani katika kuboresha sekta ya elimu nchini, hatua aliyoilezea kuwa ndiyo chachu ya maendeleo kwa sekta zote ikiwamo ya benki.

"Msaada huu unatarajiwa kuwanufaisha wanafunzi zaidi ya 300 kwa mwaka katika kipindi cha makadirio ya miaka 10. Mkakati wetu huu wa kusaidia katika elimu unatokana na imani yetu kwamba bila kuwa na jamii iliyoelimika, hata huduma za kibenki tunazozitoa lazima zitateteleka kutokana na ukweli kuwa biashara yetu hii inategemea sana mafanikio ya jamii inayotuzunguka, mafanikio ambayo tunaamini yataletwa na elimu," alisema.

Aliongeza kuwa tangu kuanza kwa mkakati huo uliozinduliwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa mwishoni mwa mwaka jana, tayari jumla ya madawati 500 yameshakabidhiwa katika mikoa ya Lindi, Dodoma, Mwanza, Mbeya na Shinyanga.

Akizungumza baada ya kupokea msaada huo, Mkuu Mkoa wa Shinyanga, Sophia, mbali na kuishukuru benki hiyo kwa msaada huo, alisema umepatikana kwa wakati mwafaka kwa kuwa mkoa huo unaendelea na mkakati wake wa kuboresha elimu kwa kuboresha mazingira ya masomo kwa wanafunzi.

"Katika kufanikisha hili Rais Samia Suluhu amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha sisi kama mkoa tunapata mahitaji yote muhimu katika elimu ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa na maslahi ya watumishi.

"Tunawashukuru sana Benki ya Exim kwa msaada huu na tunatarajia kwamba wadau wengine wataendelea kuiga mfano huu ili kwa pamoja tusaidiane kukabiliana na changamoto hii.

"Kwa sasa mkoa unakabiliwa na uhaba wa madawati 2,500 huku jitihada za kutengeneza madawati mengi zikiendelea kupitia VETA ofisi ya mkurugenzi. Hivyo, milango bado ipo wazi kwa wadau wengine kwa kuwa jitihada za pamoja ni muhimu zaidi," alisema.

# M-Pesa, benki kutoa mikopo Watanzania

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya mawasiliano ya Vodacom Tanzania imezindua kampeni ya 'Maisha yanaenda na M-Pesa' yenye lengo la kuhamasisha na kutoa elimu kwa watumiaji kuhusu huduma za utoaji mikopo kwa njia ya kidijitali zinazopatikana kwa wateja na mawakala kupitia jukwaa la M- Pesa.

Kampeni hiyo itahusisha uwezeshaji na kuhamasisha kwa kufikisha ujumbe nchini kwa muda wa miezi mitatu, Mkurugenzi wa M-Pesa, Epimack Mbeteni, akisema jana kuwa wamezidi kukua kutoka huduma ya msingi ya kutuma na kupokea pesa hadi kwenye mifumo imara ambayo sasa inatoa huduma ndogo za kifedha kwa Watanzania.

"Tumejenga mifumo bora yenye kuwezesha ufikiwaji na matumizi ya huduma jumuishi za msingi za kifedha kidijitali kama vile kutuma pesa, malipo ya bili, akiba, mikopo na pia kufanya malipo kwa simu.

"Mitazamo ya kimkakati ya Vodacom M-Pesa ni kuipeleka Tanzania katika ulimwengu wa kidijitali kwa maana kwamba tuwe na jamii isiyotumia pesa taslimu kupitia mifumo yetu mbalimbali ya kidijitali," alisema Mbeteni.

Mkurugenzi huyo aliongeza kwamba mifumo hiyo ya malipo kwa kutumia simu imeleta suluhisho la kidijitali na kuondoa hatari mbalimbali zinazoambatana na matumizi ya pesa taslimu, lakini pia M-Pesa imechangia katika huduma jumuishi za kifedha ambapo idadi ya watu wazima katika mifumo rasmi ya kifedha imeongezeka kutoka asilimia 58 (2013) hadi 65 (2017) na hivyo kuwezesha idadi ya ushirikishwaji wa kifedha nchini.

"Ukuaji wa kasi na upanuzi wa huduma za pesa kwa njia ya simu nchini ulionyesha hitaji ambalo halijatekelezwa katika sehemu ya watu wa kipato cha chini ambayo inaweza kufikiwa tu kupitia ubunifu na washirika.

"Vodacom M-Pesa imeweka ubunifu na ushirikiano muhimu na benki kama vile; NCBA Bank, TCB na FINCA ili kuwawezesha Watanzania kiuchumi kwa kutoa mikopo midogo kwa watumiaji wa M-PESA na M-PAWA na mawakala wa mtandao wa M-PESA nchi nzima," alifafanua Mbeteni.

Alisema nyenzo hizo za mikopo ni rahisi na hazina usumbufu ambapo hushughulikiwa moja kwa moja kupitia simu ya mtumiaji na hazihitaji kutembelewa ana kwa ana.

Zaidi ya hayo, alisema hiyo ni mikopo ya uhakika na ufadhili unaoungwa mkono na taasisi za fedha zinazotambulika na zinazotumia mtandao wa Vodacom Tanzania.

Alisema kwa kipindi cha promosheni, viwango vya ofa hizo vitaongezeka pamoja na kupata tokeni za LUKU bila malipo kwa watumiaji wa Songesha.

"Kipindi cha promosheni pia kitalenga kuwapatia watumiaji ujuzi wa kimsingi wa kifedha na ufahamu ambao utawaruhusu kutumia bidhaa na huduma hizi kwa manufaa ya juu zaidi. Vodacom na benki washirika zinalenga kukuza utamaduni wa kuwajibika kifedha miongoni mwa Watanzania wote," alisema.

# Hatua nne kudhibiti uvujaji wa mitihani vyuo vya afya

SAKATA la kuvuja kwa mitihani kwa vyuo vya afya limetinga bungeni huku serikali ikitaja hatua nne ilizochukua ili hali hiyo isijitokeze tena, ikiwamo kufanya mapitio ya mwongozo wa mitihani iliyo chini ya Wizara ya Afya ili kuendana na mahitaji ya kiulinzi na kiusalama.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omar Kipanga, alitaja hatua hizo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Husna Sekiboko.

Mbunge huyo alitaka kauli ya serikali kuhusu kuvuja kwa mitihani hiyo inayosimamiwa na vyuo vya afya kwa mwaka 2020.

Akijibu swali hilo, Kipanga alikiri kuvuja kwa mitihani inayosimamiwa hiyo mwezi Agosti 2021, akitaja hatua hizo kuwa ni kuboresha mfumo wa utungaji, uchapishaji na ufungaji wa mitihani kwa kushirikiana na mpigachapa wa serikali, kuongeza kasi ya uanzishwaji wa mamlaka itakayosimamia mafunzo ya vyuo vya afya ngazi ya kati pamoja na uendeshaji wa mitihani.

Alisema pia watashirikisha vyombo vya ulinzi na usalama kwenye ulinzi wa mitihani katika hatua zote kuanzia utungaji, usambazaji hadi utoaji wa matokeo.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Songwe (CCM), Philip Mulugo, alihoji hatua za serikali dhidi ya watumishi wa Wizara ya Afya waliohusika na kuvuja kwa mitihani hiyo.

"Suala la mitihani ni suala nyeti sana kwenye kila nchi, limeulizwa mara nyingi bungeni kutokana na unyeti wake, inapotokea uvujaji wa mitihani katika shule za msingi na sekondari, serikali huchukua hatua haraka ikiwamo kukamata watu na kuwafutia mitihani. Hapa mmechukua hatua gani?" Alihoji.

Mbunge huyo pia alisema suala la kuvuja mitihani ya vyuo hivyo limekuwa kimya na waliopata adha ni wazazi wa wanafunzi hao.

Kipanga akijibu swali hilo, alisema adhabu inatolewa kwa wote waliohusika na uvujaji huo.




Habari zote na Augusta Njoji



Mbunge wa Jimbo la Gairo, Ahmed Shabiby, akichangia hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Bunge lapewa taarifa upatikanaji maji Katavi

SERIKALI imeliarifu Bunge kuhusu hali ya upatikanaji wa maji katika Mkoa wa Katavi, ikibainisha kuwa kwa sasa ni wastani wa asilimia 71 kwa vijijini na asilimia 60 kwa mjini.

Naibu wa Wizara ya Maji, Maryprisca Mahundi, alibainisha hayo jana bungeni alipojibu swali la msingi la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Taska Mbogo.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji mkakati wa serikali kuhakikisha wananchi wa Mkoa wa Katavi wanapata majisafi na salama.

"Serikali ina mkakati gani wa kutumia Ziwa Tanganyika ili wananchi waweze kupata majisafi na salama?" Mbunge huyo alihoji.

Akijibu maswali hayo, Mahundi alisema kwa mwaka wa fedha 2021/22, serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maji 42 katika wilaya zote za Mkoa wa Katavi, lengo likiwa ni kuhakikisha wananchi wanapata majisafi na salama.

Alisema miradi hiyo ni pamoja na mradi wa maji Karema kwa kutumia Ziwa Tanganyika katika Wilaya Tanganyika unaotarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2022.

Vilevile, alisema Mji wa Mpanda utanufaika na utekelezaji wa mradi wa maji wa miji 28.

"Katika mwaka wa fedha 2022/23, serikali itaajiri mtaalamu mshauri wa kufanya usanifu wa kutumia chanzo cha Ziwa Tanganyika ili kuwapatia maji wananchi wa wilaya za Tanganyika, Mlele, Mpanda na maeneo ya karibu na kufikia lengo la asilimia 95 mijini na asilimia 85 vijijini ifikapo mwaka 2025," alisema.

# Bashe: Parachichi yetu inakidhi vigezo kimataifa

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amewahakikishia Watanzania na wateja wanaonunua parachichi ya Tanzania kuwa inakidhi vigezo vya kimataifa.

Pia ameagiza magari makubwa ambayo yanasafirisha parachichi pamoja na mboga kutozuiwa na badala yake yasafiri kwa saa 24.

Bashe alitoa agizo hilo jana bungeni alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Njombe Mjini (CCM), Deodatus Mwanyika, aliyetaka kujua kauli ya serikali kuhusu taarifa za mtaani zinazosema parachichi ya Tanzania siyo bora.

Akijibu swali hilo, Waziri Bashe alisema parachichi ya Tanzania inapotoka nje ya mipaka ina vyeti vyote vya kimataifa vya viwango.

"Niwahakikishie Watanzania na wateja wote, parachichi ya Tanzania inakidhi vigezo vya kimataifa na ndiyo maana tumekuwa tukifungua masoko mapya, na hivi karibuni tumefungua soko la India, na Tanzania pekee ndiyo imeruhusiwa kuingiza parachichi soko la India.

"Tuna taasisi za kimataifa zinazokubalika kwenye soko la dunia ambapo parachichi ikiondoka inakuwa na uthibitisho wa kimataifa unaokubalika kwenye soko la dunia.

"Kumekuwa na tatizo kwa washindani wetu na niwatake wasafirishaji wetu wanaposafirisha parachichi waweke 'trademark' (nembo ya biashara) kwamba hii ni bidhaa iliyozalishwa Tanzania, ushindani upo watu watataka kuharibu taswira yetu na yeyote mwenye shaka awasiliane na Wizara ya Kilimo na sisi tupo tayari kulinda bidhaa yetu popote pale," alisema.

Katika swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Ritta Kabati, alitaka kujua mkakati wa serikali kuondoa vikwazo kwa magari makubwa ambayo yanasafirisha parachichi kwenda nchi za nje.

Mbunge huyo pia alitaka kujua kauli ya serikali kuhusu kusimamisha maonyesho ya wakulima, maarufu Nanenane ambayo yalikuwa yakiwasaidia kutoa elimu kwa wakulima.

"Je, serikali inawasaidiaje wakulima wa parachichi Iringa ili waweze kulima kilimo chenye tija?" Alihoji.


Waziri Bashe, akijibu maswali hayo, alisema kuwa zao la parachichi halikuwa na mwongozo na sasa mchakato unaendelea ili kupata mwongozo mzuri kuanzia shambani mpaka sokoni.

Kadhalika, alisema kuwa ili wakulima wa parachichi mkoani Iringa wazalishe parachichi kwa tija, serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi itaendelea kuhamasisha wadau kuongeza uzalishaji wa zao la parachichi kutoka tani 190,000 mwaka 2018 hadi kufikia tani 215,000 mwaka 2022/23.

"Ili kufikia lengo hilo, serikali itaiwezesha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) kupitia Vituo vya TARI Uyole na TARI Tengeru kuzalisha miche milioni 20 itakayotosheleza eneo la hekta 114,285.72. Miche hiyo itasambazwa kwa wakulima kwa bei ya ruzuku isiyozidi Sh. 2,000 kwa mche," alisema.

Pia alisema Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI) itasimamia usajili wa wazalishaji wa miche ya parachichi na kuwapa cheti cha kuwa wazalishaji kwa lengo la kudhibiti ubora, kutoa mafunzo kwa wakulima na kuhamasisha matumizi ya miche ya parachichi iliyozalishwa kwa njia ya chupa, kujenga vituo vya huduma za pamoja na vyumba vya ubaridi katika maeneo ya uzalishaji ikiwamo Mkoa wa Iringa.

Kuhusu maonyesho, Bashe alisema kuwa kwa sasa maonyesho ya wakulima, Nanenane, yatafayika kitaifa jijini Mbeya na yatakuwa chini ya Wizara ya Kilimo na kwa upande wa kikanda yataratibiwa na ofisi za mikoa.




Ukurasa 12

**Sheria za uchaguzi kutafsiriwa njia ya kupunguza changamoto**



Ukurasa 13

PROFESA GEORGE WAJACKOYAH:
Ni mgombea urais mwenye mahaba ya gongo na bangi

siasa

JUMATANO JUNI 1, 2022

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe




Ukurasa 14

**Maji kupwaa, kujaa NCCR - Mageuzi**

# Waliotimuliwa CUF walia na Msajili Mutungi, awajibu 'sijaharibu kitu'

**Na Sabato Kasika**

SAKATA la makada 14 wa CUF waliotumbuliwa kutoka chama hicho, dhidi ya dai lao kucheleweshwa maamuzi ya malalamiko yao kutoka kwa Msajili wa Vyama vya Siasa, linachukua sura mpya.

Wakati makada hao wanaona wanacheleweshwa pasipo sababu za wazi, mtoa maamuzi Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, anasema anafuata taratibu, muda utakapowadia majibu yatapatikana.

Wana-CUF hao waliotumbuliwa baada ya kuibuka mgogoro wa kiuongozi na Mwenyekiti wao Profesa Ibrahim Lipumba, wanadai kuwa ufumbuzi wa suala lao unachelewa pasipo sababu za wazi.

Hata hivyo, wanadai kuwa hawajakata tamaa kutafuta haki yao licha ya kwamba mgogoro huo umefikisha nusu mwaka bila ufumbuzi.

Makada hao waliotimuliwa katika chama hicho ni 14, miongoni mwao akiwa ni aliyekuwa Naibu Mkurugenzi wa Habari, Uenezi na Uhusiano wa Umma, Abdul Kambaya.

Wengine ni Hamida Abdallah Huweishi aliyekuwa mgombea mwenza wa Profesa Ibrahimu Lipumba, katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Kwa mujibu wa Kambaya , wengine ni Chande Naibu Katibu Mtendaji wa Jumuiya Vijana ya CUF (JUVICUF), Ali Makame Issa, Mtumwa Ambari Abdallah, Mohamed Vuai Makame na Dhifaa Bakari ambao wote ni wajumbe wa Baraza Kuu la CUF.

Kambaya anafafanuwa kuwa yeye na wenzake wanajua mbinu zinazotumika kuwadhoofisha ili wakate tamaa kufuatilia shauri lao na kwamba hawataturudi nyuma.



Abdul Kambaya, mmoja wa makada wa CUF, waliovuliwa uanachama. **PICHA: MTANDAO**

"Tunadhani kuna mbinu mbalimbali zinafanyika za kuchelewa kutoa uamuzi ili tususe na kuwaachia nafasi wale waliotufukuza katika chama, niwaambie kuwa hatutasusa hadi kieleweke," anasema Kambaya.

Anaongeza kuwa anafahamu kuna shinikizo kubwa kutoka kwa wadau wa demokrasia linaloelekezwa kwa Ofisi ya Msajili, kutaka uamuzi wa suala lao utolewe mapema, hali inayowatia moyo kuvumilia.

**JIBU LA MSAJILI**

Kulipatia jibu hilo, Nipashe ilimtafuta Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza, ambaye amekuwa ikijuza mwenendo wa sakata hilo kila mara, jana akajibu, "naomba uongee na Msajili mwenyewe."

Pale Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, alipotafutwa kulifafanua suala hilo, akafafanua:

"Cha kwanza tunaomba isionekane kwamba Ofisi ya Msajili inaingilia vyama, ila inafanya kazi kwa utaratibu. Kinachofanyika mpaka sasa, ni mchakato na kwamba kila hatua tunayofanya tunawaarifu kila upande."

Anafafanua kuwa tatizo lililoko ni walalamikaji kuipangia muda ofisi yake wakiamini kuwa wakiwasilisha jambo lao linafanyiwa maamuzi siku inayofuata.

Jaji Mutungi anawataka walalamikaji hao kuwa na subira na kwamba Ofisi ya Msajili haiwezi kuwa sehemu ya mgogoro wao, akiwaahidi kuwa wakati ukifika uamuzi utatolewa.

**SHIDA ILIKO**

Ilikuwa Novemba mwaka jana, makada hao waliotimuliwa muda mrefu kabla katika chama hicho, waliamua kwenda Ofisi ya Msajili ya Vyama Dodoma kutafuta haki yao, dai lao likiwa ni kikao kilichowaengua hakikuwa halali.

Wanadai kufukuzwa kwao ni kukiukwa matakwa ya walichokitaja ni kukiukwa kwa Katiba ya CUF inayotaka mtuhumiwa kupewa haki ya kujitetea kabla ya kufanyiwa maamuzi.

Aidha, wanadai kuwapo na ukiukwaji wa Katiba ya CUF katika uamuzi huo, ambayo inataja haja ya kuwapo wajumbe halali wa Baraza Kuu la chama.

Hapo wanalalamika kwamba wapo, walioshiriki kupiga kura ndani ya kikao cha baraza hilo ambao kwa mujibu wa katiba hiyo hawakuwa wajumbe halali.

# Sheria za uchaguzi kutafsiriwa njia ya kupunguza changamoto




Mwananchi akipiga kura. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mroki Mroki, NEC**

SHERIA ni mfumo wa kanuni na taratibu zilizowekwa kwenye jamii na mamlaka kwa ajili ya kuongoza matendo na uhusiano wa wanajamii.

Lakini ni utaratibu unaotengeneza mfumo na mwelekeo wa maisha chini ya mamlaka zinazoongoza au kusimamia masuala mbalimbali.

Sheria zina mambo makuu matatu ambayo kila mtumiaji anapaswa kuzingatia, mosi ni lazima zitungwe na mamlaka au chombo kilichokasimiwa madaraka ya kuzitunga kwa Tanzania ni Bunge la Jamhuri ya Muungano ndilo linazozitunga.

Ni lazima sheria ziheshimiwe na kufuatwa na wote na pia zitoe adhabu kwa wanaozikiuka wakipatikana na hatia.

Kila Mtanzania anapaswa kuzijua sheria mbalimbali kwani kwa mujibu wa kifungu cha 8 cha Kanuni ya Adhabu (The Penal Code), sura ya 16 ya Sheria za Tanzania, kutokujua sheria si kigezo cha kumwondolea mtuhumiwa hatia.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) katika kutekeleza majukumu yake inaongozwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, pamoja na Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020.

Sheria hizi na kanuni zake zinazosimamia uchaguzi zimeandikwa kwa Kiingereza jambo linaloleta changamoto kwa wadau wa uchaguzi ambao hawajui lugha hiyo kwa ufasaha.

> Sheria za sasa zilizo katika lugha ya Kiingereza zinawasaidia wachache hasa wale wanaokijua na kuna watu wanaopoteza haki kwa kutofahamu lugha hiyo.

Katiba ya Tanzania ya 1977 imeandikwa kwa Kiingereza na Kiswahili.

Si tu, sheria za uchaguzi na nyingine nyingi zimeandikwa kwa Kiingereza na kuwa kikwazo kwa wananchi au watumiaji wake wengi.

Jambo hilo lilipelekea Rais wa Awamu ya tano, John Magufuli kuelekeza kutafsiri sheria zote kwa Kiswahili. Alitoa maelekezo hayo Februari 1, 2021 katika kilele cha Wiki ya Sheria na sherehe za kutimiza miaka 100 ya Mahakama Kuu ya Tanzania.

Aidha, Rais aliungwa mkono na Bunge kwa kutunga sheria ya marekebisho ya sheria mbalimbali ya mwaka 2021 inayoelekeza kuwa lugha itakayotumika katika masuala ya sheria na kuendesha mashauri mahakamani ni Kiswahili.

Lakini, NEC wakati wa kukabidhi ripoti ya Uchaguzi Mkuu wa 2020, kwenye ukurasa wa 92 iliainisha maoni iliyoyapokea kutoka katika mikutano mbalimbali ya wadau iliyofanyika nchi nzima wakati wa uboreshaji wa daftari la wapigakura na uchaguzi mkuu. Wadau walitoa maoni na mapendekezo 11 mojawapo likiwa kutaka sheria za uchaguzi kutafsiriwa kwa Kiswahili.

"Ili kuboresha zaidi shughuli za uendeshaji wa uchaguzi siku zijazo wadau wa uchaguzi pamoja na Tume wanapendekeza, pamoja na mambo mengine,...Sheria za Uchaguzi zitafsiriwe kwa Kiswahili," anasema Jaji wa Rufani mstaafu, Semistocles Kaijage katika taarifa yake, wakati huo akiwa Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Sasa NEC na taasisi zingine za serikali ipo mbioni kutafsiri Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, sura 343 na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, sura ya 292.

Tume itatekeleza takwa hilo la kuzifanyia tafsiri sheria zake za uchaguzi ili kukidhi matakwa ya matumizi ya lugha ya Kiswahili kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali ya mwaka 2021.

Kutafsiri sheria hizo kutawanufaisha watumiaji ambao ni wadau wa uchaguzi, wananchi na wanasiasa ambao mara kwa mara wamekuwa wakikumbana na changamoto wakati wa shughuli za uchaguzi kutokana na kutokuzielewa sheria za uchaguzi kwa ufasaha kwa vile zimeandikwa kwa Kiingereza.

Kutafsiriwa kwa sheria hizo kutawanufaisha wagombea, wananchi na wanasiasa kuelewa kwa urahisi na wagombea kujaza fomu za uteuzi kwa usahihi.

Tume itakapokamilisha jukumu hilo zitapitishwa zikiwa zimetafsiriwa, na wadau watazijaza kwa usahihi na kwa maana upo uwezekano wa kupunguza pingamizi wakati wa uteuzi kwa kuwa sheria zitakuwa zinaeleweka.

Katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, tume ilipokea mapingamizi mawili dhidi ya wagombea urais, 334 dhidi ya wagombea ubunge na 1,228 dhidi ya wagombea udiwani na asilimia kubwa ni kutokana na uelewa mdogo wa sheria kwa waweka pingamizi na wawekewa pingamizi.

Aidha, kutafsiriwa kutasaidia wadau wa uchaguzi kuelewa sheria na kuzifuata taratibu za michakato yake tangu hatua ya uteuzi hadi upigaji kura.

Hatua hiyo, itapunguza malalamiko kutoka kwa wadau wa uchaguzi na wananchi kwani wakati wa kutathmini uchaguzi, wadau na wananchi walieleza kukwamishwa na sheria wakijihusisha na uchaguzi.

**WADAU WAFURAHIA**

Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kaskazini, Aida Khenan (CHADEMA), anaipongeza NEC kutafsiri sheria na kusema itawawezesha wagombea na wapiga kura kuzitambua vyema sheria.

"Ni jambo jema sheria za uchaguzi zikisomeka kwa Kiswahili kwa kuwa ndiyo lugha inayotumika na kufahamika na wagombea na wapigakura," amesema Aida.

Aidha anasema sheria za sasa zilizo katika lugha ya Kiingereza zinawasaidia wachache hasa wale wanaokijua na kuna watu wanaopoteza haki kwa kutofahamu lugha hiyo.

Diwani wa Kata ya Mbuyuni, (CCM) Samuel Msuya, anasema hatua hiyo ya tume itawaamsha wanasiasa wengi wanaotaka kugombea nyadhifa mbalimbali kwa kuwa watazisoma na kuzielewa vyema sheria hizo.

Msuya anaongeza kuwa wapo watu wanachukua fomu kugombea lakini sheria hawazijui na mwishowe wanaishia katika pingamizi, lakini zikisomeka kwa Kiswahili zitawanufaisha wengi.

Diwani wa Kata ya Zuzu, Dodoma, Abdallah Awadh, anaunga mkono hatua hiyo kwasababu Kiswahili ni cha Watanzania. Hivyo, sheria zikiandikwa moja kwa moja kwa Kiswahili itakuwa jambo la tija kwa wote.

Katibu Mkuu wa Chama cha Democratic Party (DP), Abdul Juma Mluya, kwa upande wake anasema Kiswahili ndiyo lugha ya taifa, ni vyema sheria zote zikawa za Kiswahili jambo litakaloongeza uelewa wa pamoja kwa wagombea na viongozi wao.

"Sehemu kubwa ya Watanzania hawajui Kiingereza, hivyo uelewa wa pamoja katika tafsiri za sheria ulikuwa mdogo hivyo utekelezaji wa sheria hizi za uchaguzi ulikuwa wa kubahatisha miongoni mwa wagombea na hata viongozi wao," anasema Mluya.

Ni wazi kuwa sheria za uchaguzi zilizotafsiriwa zitakapokuwa tayari kwa matumizi zitawawezesha wadau kupata fursa ya kikatiba ya kuweka pingamizi, kukata rufani au kuanzisha mashauri ya uchaguzi kwa kuzingatia sheria za uchaguzi zilizotafsiriwa kwa Kiswahili.

Lakini ni wajibu wa wadau wote wa uchaguzi kufuatilia mchakato huu kwa karibu na utakapokamilika kuhakikisha wanapata nakala za sheria hizo zilizotafsiriwa na kuzisoma ili wazielewe na kuwasaidia kushiriki uchaguzi.

***Mwandishi ni Ofisa Habari Msaidizi Mwandamizi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).***

PROFESA GEORGE WAJACKOYAH:

# Ni mgombea urais mwenye mahaba ya gongo na bangi

• Aahidi kuuza bangi kulipa madeni, alia na China

**NA MWANDISHI WETU**

PROFESA George Wajackoyah, ni ingizo jipya la wagombea urais nchini Kenya, aliyeibuka mwaka huu akifichua kile kilichoko kwenye ilani ya chama chake.

Anasema ilani inalenga kuhalalisha bangi na gongo punde atakapomrithi Rais Uhuru Kenyatta na kuingia ikulu ya Kenya jijini Nairobi , Agosti mwaka huu.

Aidha, Wajackoyah anaahidi kuwaidhinisha mawaziri wakuu wanane ambao watasimamia mikoa iliyofutwa licha ya kwamba hakuitaja.

Katika ilani hiyo, mtiania huyo wa urais ambaye kitaaluma ni mwanasheria anaahidi kutoa matibabu ya bure kwa watoto, wazee na wanawake wajawazito.

Profesa George Wajackoyah, anayegombea kupitia chama cha Roots of Kenya, anapozindua rasmi ilani yake, mwanzoni mwa mwaka huu, anaeleza azma ya kuwa rais wa tano wa Kenya katika uchaguzi mkuu ujao wa Agosti 9, wenye ushindani mkali.

**BANGI Vs MADENI**

Profesa Wajackoyah, anasema atahalalisha na akiiuza bangi atatumia fedha za mauzo kulipa madeni ya Kenya, na kuilenga China ambayo imeikopesha fedha nyingi.

"Mapato kutokana na mauzo ya bangi yatasaidia kumaliza kulipa mikopo mikubwa ya kimataifa ya taifa na kisha baadaye kukata uhusiano na China, mkopeshaji mkuu wa Kenya. "

Aidha, anasema atapitia upya vibali vya kufanya kazi vya Wachina na kwamba atashika wadhifa wa kiongozi wa nchi na Waziri wa Uhamiaji, kutokana na ujuzi wake mkubwa katika sheria ya uhamiaji.

Akizungumzia bangi anaongeza kuwa wanaovuta bangi wanaishi muda mrefu zaidi na iwapo atachaguliwa rais kuvuta bangi kutakuwa ruksa.

Wakati akitangaza azma yake ya kuwania urais miezi miwili iliyopita Februari 12, katika ukumbi wa Diamond Plaza, Nairobi, alifichua kuwa atawania urais kwa tiketi ya Roots Party of Kenya.

**KAZI SIKU 4**


Profesa Wajackoyah pia anaahidi kupunguza siku rasmi za kufanya kazi nchini Kenya badala ya tano zitakuwa nne ambazo ni Jumatatu hadi Alhamisi na kwamba hilo litawaruhusu Waislamu kusali Ijumaa na Wakristo kuabudu Jumamosi na Jumapili.

Kuhusu maendeleo ya miundo mbinu , mgombea huyo anasema ataachana na mji mkuu wa Nairobi kama jiji la viwanda na kufungua jiji lingine la utawala na makao makuu ya nchi mahali pengine.

Katika ilani yake wakili huyo pia anaahidi kutibu bure watoto, wazee na wanawake wajawazito na kwamba utawala wake utaanzisha hukumu ya kifo kwa mafisadi.



Profesa Waijackoh, anayeota kuwa na taifa la wavuta bangi na wanywa chang'aa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Justina Wambui Wamae

Anaongeza kuwa punde atakapoingia madarakani katika muda wa miezi sita ya kwanza, atavunja katiba ya sasa ili kuruhusu Wakenya kuamua aina ya katiba wanayoitaka. Pia, anasema serikali yake itawapeleka watu wa kiasili kwenye makazi yao ya asili.

**POLISI WATAJWA**

Wakili huyo pia anaahidi kupiga marufuku sare za bluu za polisi na kuongeza mishahara yao mara tu atakapotwaa mamlaka.

Ana neno kwa tasnia ya habari akisema chini ya utawala wake, vyombo vya habari vitamilikiwa na wanahabari na sio wamiliki wengine. Anaongeza kuwa atahakikisha wanahabari wote wanalipwa vizuri.

Profesa Wajackoyah, amemteua Justina Wambui Wamae kuwa mgombea mwenza akiwa wa kwanza kutangaza mgombea mwenza katika historia ya Kenya, alifanya hivyo kabla ya Raila Odinga, aliyemteua Martha Karua kuwa mgombea mwenza wiki mbili zilizopita.

> Mapato kutokana na mauzo ya bangi yatasaidia kumaliza kulipa mikopo mikubwa ya kimataifa ya taifa na kisha baadaye kukata uhusiano na China, mkopeshaji mkuu wa Kenya.

Wamae anatajwa kuwa ni mhitimu wa Chuo Kikuu cha Daystar nchini humo akiwa pia na shahada ya uzamili kutoka Chuo Kikuu cha Jomo Kenyatta.

Alifahamika kisiasa kwa mara ya kwanza mwaka 2017 alipogombea ubunge wa Mavoko lakini akapoteza.

Akizungumza katika kipindi cha Meza ya Duara cha DW Jumamosi iliyopita, anasema Baraza lake la Mawaziri litakuwa na Waasia wakisimamia wizara za uchumi na mipango.

Aidha, anasema Balozi wa Kenya nchini Uingereza ni lazima awe mweye asilia ya Asia na hilo halina kipingamizi.

Na aliahidi kuwa atahalalisha unywaji wa chang'aa au gongo na kwamba kwa Kenya gongo itakuwa ruksa siyo suala la kusumbuliwa na polisi tena.

**HISTORIA YA WAJACKOYAH**

George Luchiri Wajackoyah ni mmoja wa Waafrika waliosoma zaidi ana shahada 14 na digrii kadhaa alizopatika katika vyuo vikuu vya nje na ndani ya Kenya.

Akiwa na miaka 57 hakuna Mkenya mwingine aliyefikia kiwango cha elimu na shahada alizo nazo msomi huyo.

Wajackoyah, ambaye kwa sasa anasomea Sheria ya Uhamiaji katika Chuo Kikuu cha Nairobi, anasema wao ni kwanza kuwa na kampuni ya kwanza ya mawakili katika eneo hili kufundisha sheria ya uhamiaji.

**MAISHA MAGUMU**

Profesa Wajackoyah, alizaliwa Magharibi mwa Kenya akidai alitelekezwa na wazazi wake baada ya kutalikiana akiwa na umri wa miaka 16.

Mwanasheria huyo na mwanasiasa alipata msamaria mwema aliyelipia masomo yake ya sekondari Wavulana ya St. Peter's Mumias hadi kidato cha sita.

Hata hivyo, baada ya kupanda vyeo na kutumwa kama sehemu ya usalama wa aliyekuwa Rais Mwai Kibaki, furaha yake ilikuwa ya muda mfupi.

Wakati Waziri wa Mambo ya Nje ya Kenya, Dk. Robert Ouko alipouawa Februari 12, 1990, Wajackoyah, alikuwa Inspekta wa polisi mwenye jukumu la kukusanya taarifa za kijasusi za washukiwa wauaji, lakini uchunguzi wake wa kitaalamu ulisababisha kukamatwa, kuzuiliwa na kuteswa vikali.

Bahati ilikuwa upande wake tena baada ya baadhi ya Wamarekani kumsaidia kutoka kizuizini na kumsafirisha nje ya nchi hadi Uingereza ambako alianza maisha yake uhamishoni.

Alisoma sheria na kulipia karo kwa kuchimba makaburi, na kuongeza kuwa macho yake yalikuwa mekundu kila wakati kwa sababu ya kazi ngumu na kusomo. **MITANDAO**

JUKWAA LA VIONGOZI

# Maji kupwa, kujaa NCCR-Mageuzi

- Ilianza kama 'mbuyu' wabunge 19 leo 'o'
- Yawezekana migogoro kiuongozi ina mchango

**Na Sabato Kasika**

NCCR- Mageuzi ndicho pekee kilichoibuka kwa kishindo uchaguzi mkuu wa kwanza wa mfumo wa vyama vingi 1995 kilikozoa wabunge 19 majimboni.

Hata hivyo, badala ya kuendelea kujiimarisha, kimeyumba na leo hakina hata mbunge kutokana na kugubikwa na migogoro ya uongozi, iliyoanza baada ya uchaguzi mkuu 1995.

Kabla ya kupewa jina la NCCR-Mageuzi, ilikuwa Kamati ya Kuratibu Mageuzi ya Kisiasa na Katiba (National Committee for Constitutional Reform - NCCR), Zanzibar kamati ilijulikana kama KAMAHURU, iliyoongozwa na Mwenyekiti Chief Abdallah Fundikira na wakili Mabere Marando, Katibu Mkuu.

Baadhi ya wajumbe wa kamati hiyo walikuwa James Mapalala, Mchungaji . Christopher Mtikila, Mashaka Chimoto, Ndimara Tegambwage, Dk. Ringo Tenga, Balozi Kasanga Tumbo na Kasela Bantu.

Wengine ni Prince Bagenda, huku vijana wakiwa ni James Mbatia, Anthony Komu, Idrisa Al-Nuru na Japheth Hassunga.

**MGOGORO WA KWANZA**

Kati ya Juni na Desemba 1991 kulitokea mabadiliko katika harakati za mageuzi ya kisiasa nchini, baada ya Chief Fundikira kwenda Ujerumani bila kuwataarifu Katibu na wajumbe wa kamati hiyo.

Alikwenda kwenye kongamano la kimataifa la demokrasia na siasa za vyama vingi lililofanyika Ujerumani, ambalo lilirushwa na kutangazwa zaidi na vyombo vya habari vya BBC na DW.

Lilikuwa jukwaa mahsusi kwa wanasiasa wa upinzani waliokuwa wanaibukia kudai mabadiliko na kuanzisha mfumo wa vyama vingi barani Afrika.

Aidha, wanasiasa wa upinzani wa Tanzania waliokuwa wakiishi ughaibuni, wakati huo Salathiel Kambona na Ludovick Mwijage, nao walihudhuria.

Baada ya Fundikira kurejea nchini, Marando akiungwa mkono na baadhi ya wajumbe (Bagenda, Ndimara, Chimoto na Dk.Tenga) walitaka awajibishwe kwa sababu ya kuhudhuria kongamano hilo bila kuaga na alitakiwa eleze kikao alipata wapi mamlaka ya kukusanya pesa.

Chifu Fundikira hakujibizana ila alijiondoa na kuanzisha chama Union for Multiparty Democracy (UMD), pamoja na Balozi Kassanga Tumbo, Kasela Bantu na baadhi ya wazee wakaihama NCCR.

Mparanganyiko wa NCCR uliendelea na kati ya Desemba 1991 na Februari 1992 Mapalala alijiengua na kuanzisha Chama cha Wananchi (CCW).

**KUJIPANGA UPYA**

Baada ya Chifu Fundikira na Kassanga Tumbo, wana-Kamati walimteua Mabere Marando kuwa mwenyekiti na Prince Bagenda Katibu.



Mwenyekiti wa NCCR-MAgeuzi , James Mbatia, ni shuhuda wa migogoro yote ndani ya chama ambaye leo anakabiliwa na mzozo wa kiuongozi. **PICHA: MTANDAO**

> Ilikuwa ni Septemba 22 mwaka 2015, chama hicho kilimsimamisha uongozi Makamu Mwenyekiti, Leticia Mosore kwa madai ya kukihujumu, lakini Msajili wa Vyama, Jaji Francis Mutungi alimrejesha.

NCCR iliendelea kutandaa kupitia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na machapisho, ikijitangaza magazetini na kutembelea watu maarufu wenye mwelekeo wa kimageuzi na kuwashawishi kuiunga mkono.

Aidha, Bagenda, Dk. Tenga, wanahabari Mbena Mwanatongoni na Anthony Ngaiza, Professa Mwesiga Baregu na Mashaka Chimoto, NCCR ilianzisha asasi ya kiraia ya African International Group of Political Risk Analysis (PORIS).

Jukumu la asasi hiyo lilikuwa ni kuimarisha umahiri wa kiraia (civic competence) kwa Watanzania na kueneza dhana ya mageuzi ya kisiasa.

Februari 15 mwaka 1992, Kamati ilikubaliana rasmi kuwa NCCR ibadilike kutoka Kamati ya Mageuzi ya Katiba na kuwa chama cha siasa lakini kwa kubakiza jina la NCCR na kisha kuongeza maneno Mageuzi.

Hivyo jina la chama likawa NCCR-Mageuzi Marando akiwa Mwenyekiti, Prince Bagenda Katibu Mkuu, Chimoto Katibu wa Itikadi na Uenezi, Tegambwage Katibu wa Habari na Uhamasishaji.

Chini ya timu hiyo, chama kilienea nchi nzima kwa haraka, kikibebwa na wanafunzi na wahadhiri wa vyuo vikuu na kilikunda na kuimarisha kamati za mikoa yote kikipata misaada ya hali na mali kutoka kwa wadau mbalimbali.

Wanafunzi wa elimu ya juu walifanya kazi za kueneza NCCR-Mageuzi kwa kujitolea na kikajulikana zaidi, hatua iliyokiingiza katika uchaguzi mkuu wa kwanza ndani ya mfumo wa vyama vingi kwa kishindo.

**MTIFUANO WA PILI**

Miezi michache kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 1995, Augustine Mrema, aliondoka CCM na kuhamia NCCR-Mageuzi akiwa na kundi kubwa la makada waliomfuata akiwamo mwanasiasa mkongwe Thomas Ngawaiya.

Ujio wake uliipandisha NCCR -Mageuzi na kuongeza upinzani mkali kwa CCM, kikijizolea wabunge 19 na madiwani kwenye kata nyingi kwenye uchaguzi mkuu wa 1995. Marando alimwachia Mrema uenyekiti, yeye akawa Katibu Mkuu na pia chama hicho kilimteua Mrema kuwa mgombea urais.

Baada ya uchaguzi, ulizuka mgogoro wa kiuongozi uliosababisha Mrema kujiondoa NCCR-Mageuzi na tangu wakati huo, haijasimama kama ilivyokuwa hapo mwanzo. Baada ya Mrema kuondoa, zilizuka tofauti kati ya Marando na Mbatia wakati wa kuwania nafasi ya mwenyekiti wa chama ambapo walizushiana tuhuma mbalimbali hatimaye Marando akajiondoa na kwenda CHADEMA.

Leo Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi ni Mbatia, ambaye mwaka 1992 alifukuzwa Chuo Kikuu na wanafunzi wengine tisa na kusababisha asimalize Shahada yake ya Uhandisi Ujenzi (Civil Engineering) akiwa amebakiza miezi miwili kuhitimu.

Mzoefu huyo katika siasa za mageuzi, hajawahi kuhama NCCR tangu 1992 na anaamini katika itikadi ya utu wa binadamu na ndiye ambaye na wenzake walionekana ni watukutu na vinara wa mabadiliko Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kusababisha kifungwe mwaka mmoja.

Alikuwa kiongozi wa vijana wa kwanza kipindi cha mfumo wa vyama vingi vya siasa ndani ya chama hicho, Mkuu wa Idara ya oganaizesheni, Kampeni na Uchaguzi, akifanikisha chama kupata wabunge 19, akiwa mbunge wa kwanza kijana akiwakilisha jimbo la Vunjo mkoani Kilimanjaro.

**MGOGORO WA TATU**

Ilikuwa ni Septemba 22 mwaka 2015, chama hicho kilimsimamisha uongozi Makamu Mwenyekiti, Leticia Mosore kwa madai ya kukihujumu, lakini Msajili wa Vyama, Jaji Francis Mutungi alimrejesha.

Migogoro ya uongozi ndani ya NCCR-Mageuzi ni ya muda mrefu na inawezekana ina mchango kukikosesha nguvu ya ushawishi kwa wananchi. Itakumbukwa mgogoro wa Mrema na Marando Tanga Mei 1997, ulishuhudia taa zikizimwa ghafla na viti vikirushwa na walinzi wa Mrema walifanya kazi kubwa ya kumlinda kunusuru uhai wake.

Migogoro mingine inaweza isiwe hatari kwa uhai wa chama tu bali hata kwa wanachama wenyewe, mathalani huo wa Tanga.

**MTAFARUKU WA SASA**

Mwezi uliopita bundi wa migogoro alitua tena ndani ya NCCR baada ya Halmashauri Kuu kumsimamisha Mwenyekiti Mbatia na Makamu Bara, Angelina Mtahiwa.

Hali hiyo ilisababisha makao makuu ya chama hicho Ilala Dar es Salaam kugeuka kuwa uwanja wa mapambano kwa muda kati ya wafuasi wanaomuunga mkono na wanaompinga.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu na kiranja wa maazimio ya kumng'oa, Joseph Selasini, anasema uamuzi huo umefikiwa baada ya kuwapo madai ya kuwagombanisha viongozi na kuwalazimisha kujiuzulu.

Maazimio mengine anayotaja Selasini ni pamoja kulivunja baraza la wadhamini la NCCR na kuteua wajumbe wengine, ambao watasajiliwa kwa taratibu zitakazowekwa.

Hatua hizo zilichukuliwa baada ya kikao kilichohudhuriwa na wajumbe 52 kati ya 82 waliopaswa kuwapo, lakini Katibu Mwenezi, Edward Simbeye, anadai kilichofanyika ni uhuni ndani ya chama.

Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza, wiki iliyopita ilipigilia msumari wa mwisho, akisema ofisi yake, inayolea na kusimamia vyama vyenye usajili wa kudumu, imeridhia kutumbuliwa Mbatia na sekretarieti yake na kuwataka wasijihusishe na siasa ndani ya chama hicho hadi mkutano mkuu utakapoitishwa na kuamua hatima yao.

Hata hivyo, Mbatia anaendelea kusisitiza kuwa ni mwenyekiti halali.



# Wenye ulemavu waomba kupewa elimu kuhusu sensa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WATU wenye ulemavu wa kutosikia (viziwi) mkoani hapa wameiomba serikali kuwapatia elimu ili kupata uelewa kwa vitendo itakayowasaidia kushiriki kikamilifu kwenye zoezi la uandikishaji wa sensa ya watu na makazi itakayofanyika Agosti 23, 2022.

Rai hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa Asasi ya Viziwi (DODSA), mkoani hapo, Jafari Gama, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Gama, alisema bado kuna uhitaji mkubwa kwa upande wao kwa serikali kuwafikia watu wenye ulemavu wa kutosikia na kuwapatia elimu ambayo itakayowafanya kuweze kushiriki kikamilifu katika zoezi hilo muhimu kwa taifa.

Alisema kundi hilo la watu wasiosikia bado wapo gizani na hawaelewi suala la uandikishaji wa sensa ya watu na makazi zaidi ya kuona kwenye mabango, vipeperushi na vyombo vya habari.

"Viziwi bado wanahitaji elimu zaidi itakayowawezesha kushiriki na kutoa majibu sahihi kutokana na walio wengi kuona kwenye mabango na wengine kwa kufuatilia kwenye vyombo vya habari kupitia wakalimani wa lugha ya alama," alisema.

Hata hivyo, asasi hiyo imeiomba serikali kuendelea kuwaelimisha watumishi wao kuhusu kujifunza lugha ya alama ili waweze kuwasiliana na watu wenye ulemavu huo wa kutosikia.

Alisema bado kuna changamoto kwa baadhi ya watumishi maofisini na hospitalini, vituo vya polisi taasisi za fedha na mahakama na sehemu zinginezo hakuwa wanaoweza kufafanua lugha ya alama.

Alisema watu hao wasiosikia wamekuwa wakikosa haki zao za msingi kutokana na kutokuwapo kwa mawasiliano ya lugha ya alama kwa upande wa watumishi hao.

# Watumishi wampongeza Rais Samia nyongeza mishahara

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WATUMISHI wa Umma mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa huo, Antony Mtaka, wamempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kupandisha mishahara yao kwa asilimia 23.3, posho za safari na kujikimu pamoja na kulipa malimbikizo ya madeni ya muda mrefu.

Akizungumza katika hafla fupi ya kumpongeza Rais Samia Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Antony Mtaka, aliwataka watumishi wa umma kuongeza uwajibikaji katika maeneo yao ya kazi ili kulipa fadhila zilizofanywa na serikali.

Alisema haitakuwa busara kama juhudi zilizofanywa na serikali chini ya Rais Samia za kupandisha mishahara, kuongeza posho za safari pamoja kulipa malimbikizo ya madeni zitashindwa kuleta matokeo katika utumishi wa umma.

"Wakati mheshimiwa Rais amepandisha mishahara yetu, kuongeza posho na kulipa malimbikizo ya madeni sisi watumishi tukishindwa kuleta matokeo na kuongeza uwajibikaji katika kuwatumikia wananchi wetu tutakuwa hatuja mtendea haki kabisa.

"Mimi kwa niaba ya watumishi wa mkoa wa Dodoma tunaahidi leo kuwa tutaendelea kumpa ushirikiano mheshimiwa Rais kwa kufanya kazi kwa kuzingatia sheria na kanuni na miongozo," alisema Mtaka.

Aidha, aliwataka watumishi waliobahatika kulipwa malimbikizo yao ya mishahara kuzitumia fedha hizo katika mambo yenye tija na familia zao.

"Kuna watu hapa kwenye akaunti zao wamelipwa hadi Sh. milioni 40, lakini hapa Dodoma kuna viwanja vinaunzwa milioni 2.5 wanashindwa kununua," alisema Mtaka.

Kadhalika, aliwataka watumishi kuacha kujihusisha na mambo yasiyokuwa na tija kama ulevi na anasa zisizokuwa na tija kwao.

Mwenyekiti wa Chama cha Walimu Mkoa wa Dodoma, Swamwel Malecela, alimpongeza Rais Samia kwa nyongeza ya mishahara ya asilimia 23.3 ambayo wamekuwa wakilalamikia kwa muda mrefu.

"Pamoja na nyongeza hii ya mishahara, lakini Rais Samia amefanya mambo mengine makubwa sana ikiwamo kulipa malimbikizo ya mishahara, kupandisha madaraja ya watumishi, lakini kuongeza umri wa utegemezi wa bima ya afya kutoka miaka 18 hadi 21 na katika kipindi cha miezi miwili mkoa wa Dodoma amepandisha madaraja watumishi wa kada ya uwalimu zaidi ya 2,300," alisema.

Mkuu wa Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa Tanzania (TAKUKURU), Mkoa wa Dodoma, Sostenes Kibwengo, aliwataka watumishi kutumia kiasi kilichoongezwa kwenye mishahara yao kubuni miradi itakayo waongezea kipato na kuacha kujihusisha na vitendo vya rushwa.

"Kumekuwa na dhana ya kuwa watumishi wanaomba rushwa kutokana na kipato kidogo, lakini kwa hili alilolifanya Rais mbadilike katika utumishi wenu na kubuni miradi badala ya kutumia vibaya fedha za miradi ya maendeleo," alisema Kibwengo.



Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Mary Maganga, akisikiliza maelezo kuhusu usimamizi wa soko la Majengo kwa Mkuu wa Idara ya Mazingira na Udhibiti wa Taka Ngumu wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Dickson Kimaro, wakati wa ziara ya kikazi jana kwa ajili ya kujionea jitihada za wadau katika usafi wa mazingira ambayo ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Mazingira Kitaifa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watakiwa kutumia nishati mbadala kutunza mazingira

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TAASISI za umma zimeaswa kutumia nishati mbadala ya kupikia ili kutunza mazingira.

Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Marry Maganga, alitoa ushauri huo jana jijini hapo baada ya kutembelea Chuo Kikuu Cha Dodoma (UDOM), ambacho kinatumia nishati ya gesi katika kupikia, ikiwa ni moja ya shughuli katika kuelekea maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani.

Alisema hatua hiyo ni mfano wa kuigwa katika utunzaji na uimarishaji wa mazingira kwa kuwa imeacha matumizi ya kuni na mkaa kupikia na kutumia gesi.

"Juhudi mnazozifanya za uhifadhi wa mazingira katika kuzunguka, tumeanzia jikoni tumeona nishati mbadala, kwa kweli tungekuta mikaa na kuni tungeona aibu sana, lakini tumekuta mnatumia gesi na mahala panapoandaliwa chakula pamekaa kwa usafi, hongereni sana," alisema.

Kuhusu eneo la mifumo ya kuchakata majitaka yanayotoka katika hospitali hiyo, Katibu Mkuu huyo aliipongeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) kwa kuwa na mfumo bora na wa kisasa katika kuchakata majitaka ili kulinda mazingira.

"Sisi tuna kitu kizuri ambacho tunaweza kujivunia katika suala la uchakataji wa majitaka hapa Dodoma," alisema.

Aliwataka kuhakikisha wanalinda eneo hilo ili liwe endelevu na lisiweze kuvamiwa na kutumika kwa shughuli za kibinadamu.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa DUWASA, Aron Joseph, alisema mfumo huo wa majitaka unafanya kazi kwa ufasaha mkubwa katika kuondoa takasumu pamoja na kemikali nyingine zinazoweza kuathiri mazingira.

Alisema pamoja na ufanisi wa mfumo huo, kumekuwa na wizi mkubwa wa mifuniko kwa watu wasiokuwa wema ambao mpaka sasa wamekuwa wakipambana nao.

Awali Naibu Katibu Mkuu wa Afya, Dk. Seif Shekalaghe, alisema hospitali hiyo ni miongoni mwa zinazosimamiwa na Wizara ya Afya. "Benjamin Mkapa wamekuwa ni outstanding (wakipekee) na wameset (wameweka) mfano katika baadhi ya hospitali tunazozisimamia, pamoja na kujipongeza sisi wenyewe kwa kusimamia lakini tuupongeze uongozi wa hospitali wenyewe kwa kujisimamia na kutunza mazingira,"alisema.





# USU walalamikiwa kupiga wananchi

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WANANCHI wa Kata ya Matundasi katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, wamewalalamikia maofisa wa Jeshi USU wanaolinda Msitu wa Hifadhi ya Mbiwe madai ya kuwashushia kipigo na kuwasababishia madhara.

Wananchi hao wamedai kuwa miongoni mwa madhara wanayopata ni kuvunjwa miguu, kuporwa mali zao hasa vyombo vya usafiri huku wanawake wakitelekeza watoto wao wachanga.

Walitoa malalamiko hayo juzi wakati wa mkutano wa hadhara ulioitishwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, kwa lengo la kusikiliza kero zao na waliiomba serikali kuwagawia sehemu ya msitu huo ili wautumie kwa shughuli zao.

Mmoja wa wananchi hao, Vedastus Siwiwa, alisema yeye ni miongoni mwa wananchi waliopigwa na maofisa hao baada ya kuingia kwenye msitu huo kwenda kuchimba madini ya dhahabu.

Pia, alidai mtoto wake alipigwa na kuumizwa hali iliyomfanya atumie fedha nyingi kumtibu na kuiomba serikali iwasaidie kuondoa kero hiyo iliyodumu muda mrefu.

"Mpaka sasa nimelazimika kukopa fedha nyingi kwa ajili ya kumtibu mwanangu maana baada ya kumpiga walimtelekeza, tunakuomba Mkuu wa Mkoa utusaidie ikiwezekana msimu huu tuachiwe sisi wanyonge tuendelee kufanya shughuli zetu," alisema Siwiwa.

Naye Masaka Karoli, alisema msitu huo kwa sasa umeshapoteza sifa za kuwa hifadhi kutokana na kuwa karibu na makazi ya watu na kuomba serikali iwaachie ili waendelee na shughuli zao za kiuchumi ikiwamo uchimbaji.

Alisema baadhi ya wananchi wameporwa pikipiki zao, baiskeli na vifaa mbalimbali vya kuchimbia madini huku akieleza kuwa baadhi yao wameumizwa na maofisa hao.

Alisema awali wananchi wa eneo hilo walitengewa eneo la kuchimba lijulikanalo kama Itumbi B, lakini kutokana na ongezeko la watu limekuwa dogo na kuhitaji eneo lingine litakalowatosheleza kwenye kazi zao.

"Tatizo lililoko ni kwamba huu msitu umeanzia kwenye nyumba zetu hapa, tunahitaji angalau ikiwezekana mpaka urudi nyuma kidogo ili nasi tupate sehemu ya kufanyia shughuli zetu, hapa tumeongezeka na tunahitaji maeneo kwa ajili ya kilimo, kuchungia na kuchimba," alisema Karoli.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Bosco Mwanginde, alisema msitu huo zamani ulikuwa unahifadhiwa na wananchi wa Kijiji cha Matundasi kabla ya serikali kuanzisha Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) ambao ndio wanasimamia kwa sasa.

Alisema baada ya kuanzishwa kwa wakala huo ndipo matatizo yalianza na wananchi walipigwa marufuku kuutumia msitu huo kwa shughuli zao ikiwamo kukata kuni, kuchimba madini na hata kuingia ndani ya msitu huo.

Ofisa Misitu wa TFS, Wilaya ya Chunya, Stephene Malima, alikanusha madai ya wananchi hao kupigwa akieleza kuwa hakuna sheria ya uhifadhi ambayo inawaruhusu maofisa hao kuwapiga wananchi.

Alisema kwa mujibu wa sheria za misitu, kila mtu anatakiwa kuheshimu misitu na hivyo akasisitiza kuwa wao wanalinda misitu yote waliyokabidhiwa kwa kufuata sheria.

"Kama kuna wananchi wamepigwa na wana ushahidi, ni vyema wakautoa ili wahusika wakamatwe na wachukuliwe hatua kama ilivyo kwa watu wengine lakini sisi hakuna sheria inaturuhusu kupiga watu," alisema Malima.

Baada ya kupokea malalamiko ya wananchi hao, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema kwa mujibu wa sheria hana mamlaka ya kubadili matumizi ya msitu huo na badala yake atawasilisha kwenye mamlaka zinazohusika.

Aliwataka wananchi hao kuendelea kufuata sheria wakati jambo hilo likiendelea kushughulikiwa huku akiwapiga marufuku maofisa wa TFS kuwapiga wananchi wanaoingia kwenye eneo hilo na badala yake wafuate sheria.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, akisisitiza jambo alipokuwa anazungumza na madiwani pamoja na watumishi mbalimbali wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wizi mifugo, mazao wawaibua viongozi wa kimila

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WIZI wa mazao, mifugo na uhalifu mwingine ikiwamo mauaji katika Mkoa wa Mbeya, vimewashtua viongozi wa mila ambao wamekutana kwa ajili ya kujadili njia mbalimbali za kukabiliana na matukio hayo ambayo pia wanasema yanahatarisha amani.

Viongozi hao walikutana mwishoni mwa wiki katika Tarafa ya Tembele iliyoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na kusema watatumia mbinu zao kuwadhibiti wahalifu hao.

Mmoja wa viongozi hao, Chifu Soja Masoko, alisema watatumia mbinu za kimila kuwakamata wahalifu hao hasa kuwafichua kwenye maficho yao na kuwalazimisha kujitokeza.

"Hapa leo sijasimika mkuki, lakini nawahakikishia kwamba ukitokea uhalifu nitasimika mkuki ili mhalifu ajitokeze mwenyewe, tusipofanya hivyo hali siyo nzuri na watatuhatarishia na amani.

Kwa upande wake Mkuu wa Kituo cha Polisi cha Mbalizi, Maleke Kilakala, aliwaomba viongozi hao kushirikiana na Polisi kuwafichua wahalifu hasa kwa kutumia njia za kawaida.

Aliwataka kuwahamasisha pia wananchi kutoa taarifa za siri kwa ajili ya kusaidia kuwadhibiti wahalifu kabla hawajatekeleza uhalifu wao kwa melezo kuwa kwa sasa matukio ya uhalifu yameongezeka.

# Mtaalamu mazingira ashauri matumizi jiko banifu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa kipato cha chini wameshauriwa kupika kwa kutumia majiko banifu yanayotumia kuni kidogo ili kupunguza uharibifu wa mazingira unaotokana na ukataji wa miti kwa ajili ya kuni na mkaa hasa maeneo ya vijijini.

Aidha, majiko hayo yanapunguza madhara ya kiafya yatokanayo na kuvuta hewa ya ukaa wakati wa kupika na kupunguza mabadiliko ya tabianchi ambayo yanasababishwa na kusambaa kwa hewa hiyo.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki jijini hapa na wataalamu wa mazingira wakati wa mkutano maalumu wa wadau wa mazingira uliokuwa na lengo la kuhamasisha matumizi ya majiko hayo ili kupunguza athari za kimazingira.

Mkutano huo uliwahusisha maofisa mazingira wa wilaya, maofisa misitu na wadau mbalimbali wa mazingira kutoka katika mikoa ya Mbeya na Songwe, ulioitishwa na Shirika lisilokuwa la kiserikali la Choose Water.

Meneja wa Shirika hilo, Riziki Hamisi, alisema lengo la mradi huo ni kudhibiti athari za mabadiliko ya tabia nchi ambayo yanaikabili dunia kwa sasa.

Alisema wameanza kutekeleza mradi huo katika mikoa ya Mbeya na Songwe kwa sababu wamebaini kuwa uharibifu wa misitu kwenye mikoa hiyo unaongezeka kwa kasi ikilinganishwa na maeneo mengine kutokana na matumizi makubwa ya kuni.

Alisema wanawajengea wananchi wenye uhitaji majiko hayo bila malipo yoyote kwa lengo la kupunguza kusambaa kwa hewa ukaa huku akieleza kuwa wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi ili wengi zaidi wayatumie.

"Kwenye mradi huu tunafadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Marekani C'QUEST CAPITAL ambalo ndilo linatupatia fedha za kugharamia mradi mzima, tunawahamasisha zaidi wananchi kuyatumia majiko haya kwa sababu yana msaada mkubwa," alisema Hamisi.

Meneja Mkazi wa C'QUEST CAPITAL, Gabriel Mbwalo, alisema shirika hilo kwa Afrika linafadhili miradi ya mazingira katika mataifa mengine ikiwamo Malawi, Gambia, Kenya, Zimbabwe na wanaendelea katika mataifa mengine.

Alisema pia wanafanya kazi kwenye mabara mengine ikiwamo Mashariki ya Mbali kwenye mataifa kama Malaysia, Indonesia na katika baadhi ya mataifa ya Amerika ya Kati.

Lengo la kuhimiza matumizi ya majiko hayo ni kudhibiti uzalishaji wa hewa ya ukaa duniani ambayo ina madhara kwa afya za binadamu na viumbe vingine pamoja na kusababisha athari za kimazingira.

Alisema hewa ya ukaa inazalishwa na watu wengi duniani hasa wale wa kipato cha chini kutokana na matumizi ya kuni na mkaa na kwamba hata afya zao zinakuwa matatani.

"Jiko hili linaboresha maisha ya watu wenye hali ya chini hasa wa vijijini, jiko hili linawafanya watumie muda mwingine kufanya shughuli zao badala ya kuutumia kupika maana hili jiko linaivisha chakula kidogokidogo," alisema Mbwalo.

Ofisa Mazingira wa Mkoa wa Mbeya, David Mlabwa, aliwataka wananchi kuachana na mila potofu ambazo zinawafanya wasiyakubali majiko hayo ambayo yana faida kubwa kwao.

Alisema baadhi wamekuwa wakiyahusisha majiko hayo na Freemason hali ambayo inawafanya wasiukubali huku akisisitiza kuwa mradi huo una manufaa makubwa.





## Matapeli chanzo migogoro ya ardhi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Ardhi na Makazi, Nadir Abdullatif, amesema migogoro mingi ya ardhi inasababishwa na madalali matapeli.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu hoja za wajumbe wa baraza hilo walioachangia hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake.

Nadir alisema pia migogoro hiyo huchangiwa na baadhi ya viongozi wa serikali na wa kisiasa wasio waadilifu.

Alisema serikali itatoa vibali maalum vya kuwatambua madalali ili kuepukana na madalali matapeli na kupunguza migogoro ya ardhi.

Pia alisema serikali itahakikisha inalinda haki za wananchi na pale inapotokea mwananchi kudhulumiwa kupewa haki zao.

"Sitokubali kuona wananchi wanadhulumiwa hasa katika masuala ya ardhi, lakini viongozi kuwa waadilifu katika utendaji wao," alisema.

Baadhi ya watendaji, alisema wamekuwa wakitumia jina la Rais Dk. Hussein Mwinyi katika kuwadhulumu wananchi haki zao na kuahidi kuwa viongozi hao atawashughulikia.

Aidha, Naibu Waziri huyo aliwaonya wajumbe wa baraza hilo kutojihusisha na migogoro ya ardhi bali wawe watetezi wa wananchi wanapodhulumiwa.

**"Sitokubali kuona wananchi wanadhulumiwa hasa katika masuala ya ardhi, lakini viongozi kuwa waadilifu katika utendaji wao," alisema.**

# Watoa huduma watakiwa kuonyesha bei za bidhaa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale, Simai Muhamed Said, amewataka wafanyabiashara wa maduka wa masuala ya utalii na wamiliki wa migahawa kuweka mabango yanayoonyesha bei halisi ya bidhaa wanazouza.

Simai aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, mjini Zanzibar, kutokana na kuwapo malalamiko kutoka kwa wananchi, wageni na watalii kuhusu udanganyifu unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara na watoa huduma zinazohusiana na utalii.

Alisema kuanzia Julai Mosi, mwaka huu, mfanyabiashara yeyote au mtoa huduma za utalii atakayeshindwa kuweka bayana bango linaloonyesha bei halisi za bidhaa, sheria kali zitachukuliwa dhidi yake.

"Malalamiko yao ni kuhusu kutokuwapo uwazi katika bei za bidhaa na huduma zinazotolewa ambazo husababisha utofauti wa bei ambayo hutolewa na wauza vyakula na watoa huduma. Bei hizo hutofautiana kutokana na mtu mmoja na mwingine kwa bidhaa na huduma zinazolingana," alisema.

Alisema agizo alilolitoa limesimama katika misingi ya sheria zingine za nchi zinazohusiana na utoaji wa huduma na uuzaji bidhaa ambazo zinaelekeza wafanyabiashara kufanya hivyo.

Kwa mujibu wa waziri, sheria hizo ni pamoja na ushindani halali wa biashara wa kumlinda mtumiaji Zanzibar, sheria namba tano ya mwaka 2018 na katika mwongozo wa usimamizi na uendeshaji wa bustani ya forodhani ambao tayari umeshaandaliwa kupitia agizo la wizara yake.

Pia alisema mwongozo huo uliotayarishwa kwa pamoja kati ya Mamlaka ya Mji Mkongwe, Baraza la Manispaa na Taasisi za Aga Khan ambazo ndizo zinazosimamia uendeshaji wa bustani ya Forodhani na zimeshatiwa saini.

"Katika mwongozo huo saini imetiwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Hifadhi na Uendeshaji Mji Mkongwe kwa matumizi baada ya kukutana na wadau wanaofanya biashara eneo la bustani ya Forodhani," alisema.




Naibu Waziri wa Ardhi na Makazi Zanzibar, Nadil Abdulatif, akijibu hoja za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika kikao cha bajeti kinachoendelea Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Vigezo posho kwa watumishi vyatajwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

OFISI ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, imesema malipo ya posho kwa watumishi wa umma wakiwamo watumishi wa Idara Maalum za SMZ hulipwa kwa kuzingatia nafasi, dhamana (mazingira ya kazi), cheo au taasisi anayoifanyia kazi mtumishi husika.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Wizara hiyo, Masoud Muhammed, wakati akijibu swali liliulizwa na Mwakilishi wa Pandani, Prof. Omar Fakihi, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi aliyetaka kujua ni posho ngapi zilizorekebishwa kwa mwaka huu.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilifanya uhakiki wa malipo ya stahiki kwa watumishi wa Idara Maalum za SMZ ili kujua uhalali wa malipo hayo.

Baada ya uhakiki huo, alisema serikali ilirejesha posho zote zilizokuwa zikilipwa kwa watumishi wa idara maalum kwa mujibu wa miongozo na matoleo yaliyotolewa na serikali.

"Mheshimiwa Spika, hakuna posho zilizoasisiwa au kurekebishwa kwa watumishi wa Idara Maalum za SMZ wakiwamo watumishi wa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU)," alisema.


Alisema kuhusu watumishi wa ngazi za chini kuachwa katika marekebisho, hakuna marekebisho yaliyofanyika.

Hata hivyo, alisema malipo ya posho kwa watumishi wa umma wakiwamo wa Idara Maalum za SMZ hulipwa kwa kuzingatia cheo au wadhifa na sehemu wanazozifanyia kazi (mazingira ya kazi).

"Mheshimiwa Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kulipa posho mpya na kufanya marekebisho kwa posho ambazo haziendani na hali halisi ya maisha kwa watumishi wa Idara Maalum wakiwamo wa JKU kadri hali ya uchumi itakavyoruhusu," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**LOVENESS YOSIA NTANZI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1599-0086** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya **BAOBAB mwaka 2019**, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
*Polisi taarifa DAR/MAG/RB/162411/2022*

## KUPOTEA KWA VYETI



**MIDUTA KWANGO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **INDEX NAMBA S0710-0110** kilichotolewa na Baraza la mitihani la taifa kupitia shule ya sekondari **BINZA** mwaka **2007** na cheti cha chuo chenye usajili namba namba **E0605-0022** kilichotolewa na chuo cha **NG'WANZA T.TC** mwaka **2015.** Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo cha polisi.
**POLISI TAARIFA: MOH/RB/239/2022**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**DAVID FRANCE TUMAINI** anatangaza kupotea kwa kadi yake ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 387 DAC** aina ya **TVS STAR.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **KAH/RB/190//022.**

## UNCLE MO ENTERPRISES
## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya udalali ya **UNCLE MO ENTERPRISES** kwa mamlaka iliyopewa na Mahakama ya Tanzania inatangaza nnada wa hadhara utakaofanyika tarehe 17/06/2022 saa 5 na nusu asubuhi katika kijiji cha **PANDAMBILI** katika halmashauri ya Wilaya ya **KONGWA** wa kuuza **NYUMBA HIZO ZILIZOPO NA PIKIPIKI MOJA AINA YA SUNLG ZOTE NI MALI YA NDUGU DAFFA WAZIRI MADUDU**

**NB**
> Mnunuzi atalazimika kulipa malipo ya 25% ya fedha taslimu papo hapo na 75% baada ya siku 14 toka siku ya mnada kufanyika na ukishindwa kulipa malipo yaliyobaki mnada utarudiwa na fedha ulizolipa hazitarudishwa. > Gharama za kubadilisha umiliki ni za mnunuzi mwenyewe, kumbuka vigezo na masharti kuzingatiwa.

***WOTE MNAKARIBISHWA***

**MAWASILIANO**
**0717417520, 0717073423**

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**KIZIMBANI MINING PROSPECTORS LTD.** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TRAILER yenye usajili namba T929 CCK na kadi ya gari aina ya FAO yenye usajili namba T909 DHA . Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo cha polisi .
**POLISI TAARIFA :**
**DAR/OST/RB/214647/2020**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TEMEKE kituo cha JUMUISHI mkoa D'SALAAM usimamizi wa mirathi na.1027/2022**

**Katika shauri la mirathi ya marehemu FATUMA MAKWESA SATO**


**Katika shauri la maombi ya kumteua msimamizi yaliyoletwa**

**Na.SHABANI MOHAMED SATO**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 20 mwezi 06 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia.endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa
Imetolewa leo tarehe 30 mwezi 5 mwaka 2022





**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie: 0782253676**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie: 0782253676**

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Kesi ya mauaji m'biashara J4 kusikilizwa upya

Na Richard Makore, MWANZA

MFANYABIASHARA wa mabasi Jumanne Mahende maarufu J4, aliyehukumiwa kunyongwa hadi kufa na Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mwanza kwa kosa la kuua watu wawili kwa bastola, kesi yake imeanza kusomwa upya Mahakama Kuu baada ya mtuhumiwa kukata rufani Mahakama ya Rufani Tanzania.

Mahakama hiyo iliagiza kesi hiyo ianze kusikilizwa upya Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza kwa kusomwa maelezo ya awali, kupeleka vielelezo pamoja na mashahidi.

Kesi hiyo imeanza kusikilizwa upya jana mbele ya Jaji Kassim Robert.

Akisomewa maelezo ya awali, Wakili wa Serikali, Dorcas Akyoo, alisema Julai 13, mwaka 2015, mshtakiwa anadaiwa kuwaua kwa kuwapiga risasi, Ally Mohammed Abeid na Claud Steven.

Wakili huyo alidai siku hiyo saa 4:00 usiku eneo la Nyakato, mshtakiwa ambaye ni Jumanne Mahende (45) wakati huo, aliwapiga risasi watu na kufariki dunia.

Alidai mahakamani kuwa siku ya tukio mshtakiwa aliwapigia simu watu hao na kuwaita ofisini kwake ili akawalipe deni lao.

Pia, alidai watu hao walikubali wito huo na kufika ofisini kwa mshtakiwa eneo la Nyakato jijini Mwanza.

Katika maelezo yake, wakili huyo alidai mahakamani kuwa muda mfupi baada ya watu hao kufika ofisini kwa mshtakiwa, ilisikika milio ya risasi.

Mshtakiwa anadaiwa kutumia bastola yenye namba za usajili A279104 kuwapiga risasi na baada ya tukio hilo alipiga simu polisi akidai kuwa kuna vurugu ofisini kwake.

Katika kesi hiyo shahidi wa kwanza, Aziza Steven ambaye ni mdogo wake marehemu Steven Claud, alisema siku ya tukio kaka yake alimuaga kuwa amepigiwa simu na J4 aende kuchukua hela yake.

Hata hivyo, alidai baada ya kaka yake kuondoka usiku ule hakurudi mpaka alipopigiwa simu asubuhi kwamba amefariki.

Kwa upande wake, mke wa marehemu Abeid, Dominatha Gabriel, alidai mahakamani hapo kuwa siku ya tukio, mume wake alipigiwa simu na mshtakiwa kuwa akachukue hela zake ofisini kwa J4.

Hata hivyo, alidai alipoondoka usiku ule hakurudi tena nyumbani mpaka asubuhi alipoambiwa mume wake amefariki dunia.

Kwa upande wake, aliyekuwa Mkuu wa Kituo cha polisi cha Nyakato, Almatus Muchunguzi, ambaye kwa sasa ni Mkuu wa Polisi Wilaya ya Arusha Mjini, akitoa ushahidi wake mahakamani hapo, alidai siku ya tukio mshtakiwa alimpigia simu na kumwambia kwamba ofisini kwake kulikuwa na fujo.

Baada ya kupata taarifa hiyo, alidai alituma askari kwenda eneo la tukio na walipofika usiku huo walikuta miili miwili ya marehemu ikiwa imelala chini.

Alidai baada ya kuiangalia aliona ikiwa imejaa damu na akaamua kumpigia Mkuu wa Upelelezi wa Polisi wa Wilaya ya Nyamagana ili afike kuona tukio hilo.

Kadhalika, alidai Mkuu wa Upelelezi wa Polisi wa wilaya naye alipofika alimpigia simu Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa wa Mwanza na kumhoji mshtakiwa.

Alidai kuwa mshtakiwa huyo alipohojiwa usiku ule alikiri kutenda kosa hilo na kushikiliwa na polisi kabda ya kufikishwa mahakamani kwa mara ya kwanza mwaka 2015.

Kwa upande wa utetezi uliowakilishwa na Wakili msomi, Peter Kibatala, uliwahoji mashahidi hao ili kujua ukweli wa jambo lenyewe.

Katika kesi hiyo jumla ya mashahidi 20 wanatarajia kutoa ushahidi wao pamoja na vielelezo tisa kuwasilishwa mahakamani hapo.

Jumla ya mashahidi wanne jana walitoa ushahidi wao mbele ya mahakama hiyo na Jaji Kassim Robert aliahirisha kesi hiyo hadi leo kwa mashaidi wanne kuendelea kutoa ushahidi wao.

## SUMAJKT yaandikiwa barua kusudio kufunguliwa mashtaka

Na Grace Gurisha

KAMPUNI ya Uwakili ya RK Rweyongeza & Co, imeliandikia Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT) kusudio la kulifungulia mashtaka kwa kosa la kuidharau Mahakama kwa kuingia mkataba na kampuni ya Bansons Enterprises Ltd, kwa ajili ya ulinzi wa kiwanja ambacho Mahakama ya Rufani iliamuru kusimamisha utekelezaji.

Kutokana na uamuzi huo wa Mahakama, kiwanja hicho kiliendelea kubakia katika himaya ya Kampuni ya J.W.Ladwa (1977) Ltd, na barua hiyo iliandikwa Mei 25, 2022 na kupokelewa SumaJKT Mei 26, mwaka huu.

Kampuni hiyo ilimwandikia barua Mkurugenzi Mtendaji wa SUMAJKT, kwa kuwa mteja wao, ambaye alikuwa mdaiwa alishindwa katika Mahakama Kuu ya kwamba alichukua hatua muhimu kuhusiana na mchakato wa kukata rufaa Mahakama ya Rufani.

Wakati wa majaribio ya kumuondoa mteja wao katika kitalu namba 273 bloku C, Chang'ombe Dar es Salaam yalipoanza, mteja wao aliomba na akapata amri ya kusimaisha utekelezaji, kwa maana mshinda tuzo (Bansons) alizuiwa kumuondoa mteja wao kutoka katika eneo hilo lililotajwa.

Mwaka 2017 Kampuni ya Bansons, ilifungua kesi ya ardhi namba 3 ya mwaka 2017, Mahakama Kuu Masjala ya Dar es Salaam dhidi ya J.W.Ladwa (1977) Ltd kuhusiana na kiwanja katika kitalu namba 273, bloku C, eneo la Chang'ombe, jijini Dar es Salaam.




Mkurugenzi wa Wateja Wadogo na Wakati wa Benki ya CRDB, Boma Labala (wapili kulia), Ofisa Mtendaji Mkuu wa Startimes, Luo Hao (wapili kushoto), Meneja Masoko wa Strategies, Lilian Suka (kulia) kwa pamoja wakimkabidhi mfano wa zawadi ya bima ya Safari za Miss Tanzania 2022 za nje ya nchi, Halima Kopwe, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mpango mpya elimu wapongezwa, TCU yabariki

Na Mwandishi Wetu

WADAU wa elimu ya juu wamepongeza mpango mpya wa serikali kuvitaka vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu kuanzisha kampasi katika maeneo mbalimbali ili kupanua wigo wa elimu.

Wakizungumza wakati wa mahojiano na mwandishi wa habari hii kwa nyakato tofauti, wadau hao walisema mpango huo utawezesha upatikanaji wa wahitimu wenye ujuzi na wanaohimili ushindani wa soko la ajira unaokuwa kwa kasi.

"Tunaipongeza serikali kwa kuwa na mpango wa kupanua wigo wa elimu ya ufundi kwa kuvitaka vyuo vikuu na taasisi zingine za elimu ya juu kufundisha kozi zinazotoa ujuzi kwa wahitimu ili waweze kustahimili ushindani wa soko la ajira," alisema Angela Mungai, mdau wa elimu wakati wa mahojiano kuhusu elimu ya juu Tanzania.

Maoni hayo ya wadau yanatokana na tamko la Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alilotoa bungeni hivi karibuni, akihamasisha vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu kuanzisha kampasi za elimu ya ufundi kama sehemu ya mkakati wa muda mrefu wa kuboresha utoaji wa elimu, inayowapa wahitimu uwezo wa ushindani watakao utumia katika soko la ajira nchini.

Akihitimisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo, Prof. Mkenda aliliambia Bunge kuwa serikali imeweka mpango mkakati kuhamasisha vyuo vikuu kujenga kampasi za elimu ya ufundi katika mikoa mbalimbali nchini.

Pamoja na mambo mengine, Prof. Mkenda alisema mpango huo unakusudia kukuza utoaji wa elimu ya ufundi katika vyuo vikuu na taasisi zingine za elimu ya juu kwa kuwajengea wahitimu uwezo kwa kuwapa ujuzi unaotakiwa kwenye soko la ajira la dunia ya leo.

Waziri Mkenda alikuwa akijibu maswali ya muda mrefu ya wabunge na wadau wa elimu ya juu, ambao kwa nyakati mbalimbali wamekuwa wakionyesha haja ya kuwapo kwa vyuo vikuu na taasisi zingine za elimu ya juu kutoa wahitimu wenye ujuzi unaotakiwa kwenye soko la ajira lenye ushindani mkubwa.

"Soko la ajira linahitaji wahitimu wenye ujuzi wa kazi na si tu kuwa na shahada zinazoonyesha ufaulu mzuri. Tunafurahi kuona serikali imedhamiria kupanua wigo wa elimu ya ufundi hadi vyuo vikuu na taasisi zingine za elimu ya juu," alisema Mohamed Unju, mbobezi katika elimu ya juu.

Hata hivyo, wadau walisema mpango huo mpya wa serikali hautazaa matunda kama Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) haitarekebisha miongozo yake, wakitaja kifungu 1.5 cha Mwongozo wa Elimu ya Juu Tanzania (Toleo la 3) la mwaka 2019 kama ni kikwazo kitakachovizuia vyuo vikuu kutenga kampasi za elimu ya ufundi kama inavyoelekezwa katika mpango mpya uliotangazwa na waziri mwenye dhamana bungeni.

"Wakati umefika sasa kwa TCU kupitia mwongozo huu na kuviruhusu vyuo vikuu na taasisi zingine za elimu ya juu kutoa kozi zinazowapa wahitimu ujuzi unaoendana na soko shindani la ajira la dunia ya leo, mpango mpya wa serikali, ukuaji wa uchumi na mikakati ya maendeleo," alisema mbobezi wa masuala ya elimu, Joseph Mfutakamba.

# NTIBAZONKIZA KUIBUKIA USAJILI SINGIDA BIG STARS

**Na Saada Akida**

WAKATI Yanga ikimpa mkono wa kwa heri nyota wake, Saidi Ntibazonkiza, mshambuliaji huyo anatarajiwa kuwa sehemu ya kikosi cha Singida Big Stars (DTB FC), kwa ajili ya kukiimarisha kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, imefahamika.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Idara ya Habari na Mawasiliano ya Yanga, Ntibazonkiza amemaliza utumishi wake ndani ya klabu hiyo baada ya mkataba wake kufikia tamati.

Juzi kwenye mtandao huo, klabu hiyo ilitoa taarifa ya kuachana na mchezaji huyo raia ya Burundi, baada ya mkataba wake wa miaka miwili kumalizika Mei 30, mwaka huu.

Lakini akizungumza jana, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli alisema kuwa mkataba na Saido umekwisha na wameshindwa kuendelea naye kutokana na pande zote mbili kushindwa kuafikiana masharti ya mkataba mpya waliotaka kuingia.

"Mkataba umeisha, tumekaa kupeana masharti ya mkataba, kila mmoja, klabu na mchezaji ulitoa masharti ya mkataba mpya, kila upande ukaona kwamba hauwezi kuutekeleza, basi tukaagana, nadhani hapo hakuna jipya wala cha ajabu," alisema Bumbuli.

Hata hivyo, taarifa zilizofikia gazeti hili kutoka kwa mtu wa karibu ndani ya Bodi ya Klabu ya Singida Big Stars, nyota huyo ameingia katika mipango ya kusajiliwa na timu hiyo iliyopanda Ligi Kuu huu. Alisema Saido amekuwa na uwezakano mkubwa wa kusajiliwa na kwenda kuitumikia timu hiyo kwa sababu kwa sasa ni mchezaji huru na tayari mazungumzo ya siri yanaendelea kati yake na kigogo mmoja mkubwa ndani ya timu hiyo.

"Singida Big Stars wako katika usajili mkubwa na mmoja wa wachezaji watakaosajiliwa ni Saido kwenda kuongeza nguvu ndani ya timu hiyo kwa ajili ya kuleta ushindani msimu ujao wa Ligi Kuu na michuano mingine itakayokuwa mbele yao," alisema kigogo huyo ambaye hakutaka kuweka jina lake.

Gazeti hili lilimtafuta Mtendaji Mkuu wa Singida Big Stars, Muhibu Kanu, ambaye alisema hawezi kuzungumzia suala la usajili kuhusu nani anaingia na kutoka kwa sababu kwa sasa bodi inapitia kwanza ripoti na tathmini ya msimu wa Championship waliomaliza.

Alisema wamejipanga kuhakikisha wanaimarisha kikosi cha timu hiyo kwa kufanya usajili mzuri kwa ajili ya kuleta ushindani mkubwa katika ligi na mashindano mengine yatakayokuwa mbele yao.

"Usajili utafanyika mzuri na watasajiliwa wachezaji wazuri na wenye kuleta ushindani mkubwa katika ligi na kuhakikisha haturudii makosa ya misimu iliyopita kwa kushusha daraja Singida United (iliyobadilishwa jina na kuitwa DTB FC na sasa Singida Big Stars)," alisema Kanu.




Mwenyekiti wa Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA), Dk. Devotha Marwa (wa tatu kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mhariri wa Michezo wa gazeti la Nipashe, Isaac Kijoti (wa pili kulia), alipotembelea katika chumba cha habari cha Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL), inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Mikocheni, Dar es Salaam jana. Wengine ni Mhariri Mtendaji wa gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe (kulia), Makamu Mwenyekiti wa CHANETA, Shyrose Bhanji (wa tatu kulia), Mjumbe wa Kamati Tendaji ya chama hicho, Shukuru Kiwege (wa pili kushoto) na Mpigapicha Mkuu wa TGL, Seleman Mpochi. **PICHA: JOHN BADI**

## Geita Gold yaanza kuiwinda Dodoma Jiji

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha timu ya Geita Gold FC, leo kinaanza mazoezi rasmi ya kujiandaa kukutana na timu ya Dodoma Jiji FC Juni 7, mwaka huu baada ya kupewa mapumziko mafupi.

Akizungumza na gazeti hili jana kwa njia ya simu kutoka mkoani Geita, Kocha Mkuu wa Klabu hiyo, Fred Filex Minziro, alisema aliwapa mapumziko mafupi wachezaji tangu walipomaliza mchezo dhidi yao na timu ya Tanzania Prisons, ambao walitoka sare.

**"Kesho (leo), tunatarajia kuanza mazoezi kwa lengo la kujiandaa kukutana na timu ya Dodoma Jiji, lengo ni kupata pointi tatu kwenye mchezo huo ili kufikia malengo yetu ya kumaliza nafasi za juu," alisema Minziro.**

Alisema anaupa umuhimu mchezo huo kwani watakuwa kwenye uwanja wa nyumbani na wanapaswa kupambana kufa ama kupona.

Alisema mchezo huo utakuwa mgumu na wa ushindani na kudai makosa ya kimchezo aliyoyabaini kwenye mchezo uliopita atayafanyia kazi ili yasijitokeze kwa mara nyingine.

Kocha huyo alisema Ligi Kuu ya NBC msimu huu ina ushindani mkali kwa kile alichokisema kuwa mpaka sasa hakuna timu ambayo imepata uhakika wa kushika nafasi ya tatu na kwamba kila siku matokeo yanabadilika kutokana na ushindani uliopo.

Minziro aliomba mashabiki wao waendelee kuwaunga mkono ili wafanye vizuri katika michezo yao yote iliyobakia na kufikia malengo yao.

Geita Gold ilipo katika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na alama 36, moja nyuma ya Namungo FC na Azam zinazoshika nafasi ya tatu na nne.

# CHANETA na mkakati mpya kuinua netiboli

**Na Adam Fungamwango**

CHAMA cha Netiboli nchini (CHANETA), kimeahidi kuuinua tena mchezo huo na kuurejesha umaarufu wake kama ilivyokuwa zamani.

Wakizungumza jana kwenye ofisi za gazeti hili walipofanya ziara ya kutembelea Kampuni ya Magazeti ya The Guardian, viongozi wa chama hicho wamesema kwa sasa wameanza kazi kubwa ya kuurudisha mchezo huo kwenye chati na kwa kuanzia, wanaanza kwa kuanzisha mashindano mbalimbali ya mitaani, shuleni, taasisi na vyuo ili kuibua vipaji vipya kwa ajili ya manufaa ya baadaye.

Viongozi waliofanya ziara hiyo ni Mwenyekiti, Dk. Devota Marwa, Makamu Mwenyekiti, Shyrose Bhanji na Mjumbe wa Kamati ya Utendaji, Shukuru Kiwege.

Viongozi hao walikuwa kwenye ziara ya kujitambulisha baada ya kukamilika kwa uchaguzi wa chama hicho kwenye baadhi ya nafasi zilizokuwa wazi hivi karubuni.

"Tuna mambo mengi ya kufanya, kwanza tukitambulishe chama kwa sababu ni kama vile kilikuwa kimepotea, netiboli nayo imepotea, tunataka kuweka ushirikiano mzuri kwenye vyombo vya habari, wadau na taasisi mbalimbali, wachezaji na hata wazazi ili kuuhamasisha tena mchezo huu.

"Tunataka kuibua vipaji vya wachezaji kutoka chini, tunataka kuanzisha ligi za mitaani, shuleni, taasisi ili kuurejesha mchezo huo kule ambako ulikuwa kwenye miaka ya nyuma," alisema mwenyekiti wa chama hicho.

Mbali na kuinua vipaji, ikiwa ni pamoja na kuurudisha tena mchezo huo kwenye chati, alisema mkakati wao mwingine ni kuboresha na kutengeneza miundombinu.

"Pale ambapo hakuna, tunatengeneza na kama ipo basi tunaboresha miundombinu, lengo ni kuwa na kiwanja cha netiboli angalau kila mkoa, kujenga ofisi bora ya CHANETA kwa sababu hii ya sasa haina hadhi ya taasisi yenyewe, lakini tuna mpango wa kujenga hosteli ambayo mbali ya kuwaweka wachezaji wa timu ya taifa, lakini itakuwa kama kitega uchumi chetu, kwani pamoja na kutafuta wafadhili na wadhamini, lakini tunatakiwa pia kuwa na sehemu ambayo itatuingizia pesa, kwa kukodisha pale watu watakapotaka kuitumia," alisema Dk. Marwa.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### TIMBER AWANIWA UNITED

KLABU ya Manchester United imeanza mazungumzo ya kumsajili beki wa kimataifa wa Uholanzi, Jurrien Timber mwenye umri wa miaka 20, anayeichezea Ajax ambaye thamani yake ni pauni milioni 43. ***(Mirror)***

### MANE HAJAIAMBIA LIVERPOOL

MSHAMBULIAJI wa Senegal, Sadio Mane mwenye umri wa miaka 30, hajaiambia mpaka sasa Liverpool kwamba anataka kuondoka katika klabu hiyo huku kukiwa na tetesi za kutaka kuhamia kwa mabingwa wa Bundesliga, Bayern Munich kwa pauni milioni 35. ***(Sky Sports).***

### NUNEZ NA VIGOGO EPL

MSHAMBULIAJI wa Benfica, Darwin Nunez mwenye umri wa miaka 22, amekuwa akikutana na baadhi ya timu kubwa za Ligi Kuu England kuhusu uwezekano wa kuhama katika majira haya ya joto. Liverpool, Manchester United na Newcastle zote zinavutiwa na raia huyo wa Uruguay. ***(Mail)***

### CUCURELLA AFUATILIWA CITY

KLABU ya Manchester City inafuatilia kumsajili beki wa kushoto wa Brighton, mwenye umri wa miaka 23, Marc Cucurella na kiungo wa kati wa Leeds na England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 26. ***(Telegraph).***

### ARSENAL KWA RICHARLISON

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Richarlison anafikiria mustakabali wake pale Everton, huku Chelsea, Tottenham na Arsenal wakionyesha nia ya kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Mail)***

### LUKAKU NA HATIMA YAKE

MSHAMBULIAJI wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 29, pia anapanga kufanya mazungumzo na Chelsea kuhusu mustakabali wake ndani ya kikosi hicho. ***(Sky Sport)***

### WEST HAM KUMUUZA DIOP

WEST Ham ipo tayari kumuuza beki Mfaransa, Issa Diop, 25, ambaye kwa sasa amekuwa chaguo la nne chini ya kocha, David Moyes. ***(Mirror)***

### NELSON AMULIKWA CITY

MABINGWA wa Ligi Kuu England, Manchester City wanamfuatilia beki wa Leicester City, Ben Nelson, 18. ***(Mail)***

### TCHOUAMENI ATAKIWA MADRID

REAL Madrid wameendelea kuweka juhudi zao za kutaka kumnunua kiungo wa kati wa Monaco, Aurelien Tchouameni, 22, kwa dau la takribani pauni milioni 68. ***(Marca)***

### WINKS AFIKIRIWA SEVILLA

KLABU ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Sevilla inafikiria kujiunga katika mbio za kumsajili kiungo wa kati wa Tottenham Hotspur na England, Harry Winks, 26. ***(Sun)***

### WILLIAN KUREJEA ULAYA

WINGA wa zamani wa Chelsea na Arsenal, Willian, 33, anatamani kuondoka nchini kwao Brazil, ambako kwa sasa anaichezea Corinthians, na kurejea kucheza soka Ulaya. ***(Fabrizio Romano)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# LEWANDOWSKI AMTIBUA KAHN KUTANGAZA KUONDOKA BAYERN

## Kwa nini alichagua njia hii, siwezi kukuambia, kauli kama hizi hadharani hazikufikishi popote...

**MUNICH,** Ujerumani

MTENDAJI Mkuu wa Bayern Munich, Oliver Kahn amemkosoa mshambuliaji nyota, Robert Lewandowski kwa kuficha hadharani nia yake ya kutaka kuondoka katika klabu hiyo.

**Lewandowski ambaye alijiunga na Bayern mwaka 2014 kwa uhamisho wa bure kutoka Borussia Dortmund - haoni nafasi yoyote ya baadaye pale Bayern, akisema muda wake katika klabu hiyo umekwisha.**

Raia huyo wa Poland ameisaidia Bayern kushinda mataji nane mfululizo ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, pamoja na Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2020.

Hata hivyo, mkataba wake unaisha ndani ya muda wa mwaka mmoja tu, na Lewandowski anaripotiwa kutaka kujiunga na Barcelona katika dirisha hili la uhamisho.

Akizungumza katika mkutano na wanahabari kabla ya Ligi ya Mataifa ya Uefa, Lewandowski alisema: "Sipendi kuwa katika hali hii. Kilicho hakika kwa sasa ni kwamba muda wangu pale Bayern umekamilika. Sioni nafasi yoyote ya kuendelea katika klabu hii."

Msimu uliopita, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, alivunja rekodi ya Gerd Muller kwenye Bundesliga ya kufunga mabao 40 katika msimu mmoja, na safari hii amefunga mabao 50 katika mashindano yote kwa wababe hao wa Bavaria.

Kahn alifichua hisia zake kuhusu suala hilo kupitia SPORT1 Jumatatu, akisema: "Kwa nini Robert alichagua njia hii, siwezi kukuambia. Kauli kama hizi hadharani hazikufikishi popote.

"Robert amekuwa (mchezaji bora wa mwaka wa FIFA) hapa mara mbili mfululizo - nadhani anapaswa kujua alichonacho FC Bayern."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT
TZS. 233,

MECHI KALI
ITALY
VERSUS
ARGENTINA
1 | 2.77
X | 2.97
2 | 2.48

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MESSI AMPA BENZEMA BALLON D'OR



**PARIS,** Ufaransa

LIONEL Messi amesema "hakuna mashaka" Karim Benzema atakuwa mshindi wa tuzo ya Ballon d'Or baada ya nyota huyo wa Real Madrid kuisaidia timu yake kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.


Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa ndiye anayepewa nafasi kubwa ya kurithi mikoba ya Muargentina huyo kama mpokeaji mwingine wa tuzo ya mtu binafsi yenye hadhi ya juu katika mchezo huo baada ya kuiwezesha timu yake kupata mafanikio ya ndani na Ulaya msimu huu.

Benzema alifunga mabao 44 katika michezo 46 kwenye michuano yote msimu huu kwa kikosi hicho cha kocha, Carlo Ancelotti na kukiongoza mjini Paris kuifunga Liverpool Jumamosi akiwa nahodha.

Messi, ambaye ameongeza kwenye kabati lake mataji kwa kunyakua taji la Ligue 1 akiwa na Paris Saint-Germain katika mwaka wake wa kwanza nje ya Barcelona, bila shaka anahisi Benzema atapata tuzo hiyo.

"Nadhani hakuna mashaka," alisema Messi akiiambia TyC Sports alipoulizwa kama Mfaransa huyo angekuwa mrithi anayefaa kama mshindi wa Ballon d'Or. "Ni wazi kwamba, Benzema alikuwa na mwaka mzuri na amefanya vizuri kwenye Ligi ya Mabingwa, ambayo ilikuwa msingi kutoka kwenye hatua ya 16 na kuendelea katika michezo yote.

"Nadhani hakuna shaka mwaka huu."



## City kusajili zaidi msimu huu

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City inatarajia kuongeza wachezaji "wengi" zaidi baada ya kunasa saini za Erling Haaland na Julian Alvarez, Mwenyekiti Khaldoon Al Mubarak, amethibitisha.

Wakiwa wamelitwaa taji lao la nne la Ligi Kuu England katika kipindi cha miaka sita kwa ushindi mnono, siku ya mwisho dhidi ya Aston Villa, City wanatatarajiwa kufaidika kwa kumnunua nyota wa Norway, Haaland, ambaye alifunga mabao 86 katika mechi 89 katika kipindi cha miaka miwili akicheza kule Borussia Dortmund.

Vijana hao wa kocha, Pep Guardiola pia walitangaza kumsajili mshambuliaji mchanga kutoka River Plate, Alvarez Januari, huku City wakitarajia kurekebisha safu yao ya mbele mwaka mmoja baada ya kuondoka kwa gwiji wa klabu hiyo, Sergio Aguero.

Wakiwa tayari wamegonga vichwa vya habari kuhusu biashara yao ya uhamisho, hasa kwa kumsajili Haaland - El Mubarak, amesema wanatarajia kuimarisha zaidi kikosi hicho.

"Ninaweza kuthibitisha kwamba, kutakuwa na wachezaji zaidi wanaokuja," El Mubarak aliiambia tovuti ya klabu. "Tunatafuta kuimarisha timu katika maeneo ambayo tunahitaji kuimarishwa.




# 880,320

## JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 01/06/22 | 21:45 | Scotland vs Ukraine | 2.27 | 3.13 | 3.33 |
| 02. 01/06/22 | 21:45 | Italy vs Argentina | 2.82 | 3.02 | 2.41 |
| 03. 03.06.22 | 00:00 | Real Cartagena vs Leones FC | 2.68 | 3.02 | 2.53 |
| 04. 02.06.22 | 02:30 | Fortaleza CE vs Ceara CE | 2.24 | 3.16 | 2.97 |
| 05. 02.06.22 | 02:30 | USA vs Morocco | 2.24 | 3.18 | 3.33 |
| 06. 02.06.22 | 03:30 | CRB AL vs CSA AL | 2.39 | 2.91 | 2.96 |
| 07. 02.06.22 | 19:00 | Bulgaria vs North Macedonia | 2.54 | 2.98 | 2.93 |
| 08. 02.06.22 | 19:00 | Cyprus vs Kosovo | 3.25 | 3.15 | 2.25 |
| 09. 02.06.22 | 21:45 | Czech Republic vs Switzerland | 2.90 | 3.25 | 2.39 |
| 10. 02.06.22 | 21:45 | Spain vs Portugal | 2.24 | 3.25 | 3.15 |
| 11. 02.06.22 | 21:45 | Serbia vs Norway | 2.27 | 3.10 | 3.25 |
| 12. 02.06.22 | 21:45 | Slovenia vs Sweden | 3.21 | 3.11 | 2.29 |
| 13. 02.06.22 | 21:45 | Northern Ireland vs Greece | 2.85 | 3.00 | 2.60 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATANO - 01/06/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2446 | Gamba Osaka vs Gifu | 1.20 | 5.84 | 10.71 |
| 13:00 | 3686 | Niigata Albirex vs Roasso Kumamoto | 1.68 | 3.46 | 4.68 |
| 13:00 | 3878 | Mito Hollyhock vs Renofa Yamaguchi | 1.82 | 3.32 | 4.00 |
| 13:00 | 4981 | JEF United Chiba vs Zwiegen Kanazawa | 1.92 | 3.12 | 3.85 |
| 13:00 | 5234 | V Varen Nagasaki vs Kagoshima United | 1.62 | 3.65 | 4.76 |
| 13:00 | 5896 | Urawa Red Diamonds vs Fukushima Utd | 1.22 | 5.44 | 10.70 |
| 15:00 | 2256 | Panama Youth vs Argentina Youth | 4.89 | 3.91 | 1.56 |
| 16:00 | 1198 | Australia U23 vs Kuwait U23 | 1.30 | 4.78 | 8.38 |
| 16:00 | 1766 | Banik Ostrava B vs Viktoria Otrokovice | 1.28 | 5.64 | 7.00 |
| 16:00 | 1787 | Galatasaray U19 vs Atiker Konyaspor U19 | 1.46 | 4.29 | 5.46 |
| 16:00 | 2016 | Altay U19 vs Fatih Karagumruk U19 | 2.58 | 3.41 | 2.39 |
| 16:00 | 2316 | Istanbul Basaksehir AS U19 vs Besiktas JK U19 | 3.41 | 3.46 | 1.93 |
| 16:00 | 2452 | Balikesirspor U19 vs Bursaspor U19 | 2.22 | 3.21 | 2.97 |
| 16:00 | 4621 | Trabzonspor U19 vs Fenerbahce U19 | 2.04 | 3.60 | 3.02 |
| 16:00 | 5289 | Tuzlaspor U19 vs Bandirmaspor U19 | 2.73 | 3.36 | 2.30 |
| 16:00 | 5395 | Belarus U21 vs Cyprus U21 | 2.18 | 3.27 | 2.97 |
| 16:00 | 5916 | Iran U23 vs Qatar U23 | 2.14 | 2.96 | 3.39 |
| 17:00 | 5780 | Kasimpasa U19 vs Goztepe U19 | 1.56 | 3.98 | 4.76 |
| 18:00 | 1600 | Loko Vltavin vs Slavoj Vysehrad | 1.66 | 3.91 | 4.11 |
| 18:00 | 1927 | Viktoria Plzen B vs Karlovy Vary | 1.56 | 4.08 | 4.66 |
| 18:00 | 2401 | SK Rakovnik vs Slavia Prague B | 6.21 | 5.05 | 1.35 |
| 18:00 | 2613 | Usti N Orlici vs Slovan Liberec B | 3.65 | 3.46 | 1.86 |
| 18:00 | 2630 | Enyimba vs Sunshine Stars FC | 1.53 | 4.10 | 4.89 |
| 18:00 | 2955 | SK Zapy vs Sokol Brozany | 1.48 | 4.41 | 5.09 |
| 18:00 | 4332 | FK Prepere vs Mlada Boleslav B | 1.56 | 4.47 | 4.28 |
| 18:00 | 4412 | Shooting Stars vs Remo Stars | 1.70 | 3.90 | 3.90 |
| 18:00 | 4640 | Akwa United vs MFM FC | 1.43 | 4.50 | 6.60 |
| 18:00 | 5070 | Hradec Kralove B vs Jablonec B | 2.63 | 3.80 | 2.19 |
| 18:00 | 5116 | Admira Prague vs Pisek | 2.49 | 3.37 | 2.49 |
| 18:00 | 5134 | FK Zbuzany vs Slovan Velvary | 2.40 | 3.55 | 2.48 |
| 18:00 | 5157 | Rivers United FC vs Plateau United | 1.44 | 4.67 | 5.25 |
| 18:00 | 5310 | Fastav Zlin B vs Blansko | 1.74 | 3.65 | 3.99 |
| 18:00 | 5724 | Pardubice B vs Teplice B | 1.74 | 4.48 | 3.31 |
| 18:30 | 3973 | France U18 vs Saudi Arabia Youth | 1.26 | 5.08 | 9.18 |
| 18:30 | 4734 | Uzbekistan U23 vs Turkmenistan U23 | 1.12 | 6.58 | 17.42 |
| 18:45 | 4784 | MC Oran vs JS Saoura | 2.73 | 2.83 | 2.63 |
| 18:45 | 5835 | CS Constantine vs ES Setif | 4.08 | 3.50 | 1.76 |
| 19:00 | 1765 | KS Blonianka Blonie vs KS Pelikan Lowicz | 2.58 | 3.31 | 2.44 |
| 19:00 | 1768 | SK Benesov vs Motorlet Prague | 2.67 | 3.25 | 2.39 |
| 19:00 | 1844 | Jiskra Domazlice vs FK Stechovice | 1.37 | 4.87 | 6.03 |
| 19:00 | 3272 | Banik Sokolov vs Hostoun | 2.20 | 3.69 | 2.67 |
| 19:00 | 3371 | Mlks Wissa Szczuczyn vs Legionovia | 15.53 | 7.57 | 1.11 |
| 19:00 | 4065 | Pribram B vs Kraluv Dvur | 3.75 | 3.60 | 1.80 |
| 19:00 | 5244 | Poland vs Wales | 1.80 | 3.46 | 4.41 |
| 20:00 | 2626 | Jordan U23 vs Iraq U23 | 2.84 | 2.89 | 2.49 |
| 20:00 | 3369 | Australia vs Jordan | 1.74 | 3.49 | 5.05 |
| 20:00 | 5133 | Faroe Islands U21 vs Ukraine U21 | 7.21 | 4.38 | 1.36 |
| 21:45 | 1649 | Scotland vs Ukraine | 2.33 | 3.07 | 3.28 |
| 21:45 | 4468 | Italy vs Argentina | 2.77 | 2.97 | 2.48 |
| 22:00 | 2568 | Tenerife vs Las Palmas UD | 2.45 | 3.03 | 2.93 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# WATANZANIA WOTE WAITWA KUSHUHUDIA KOMBE LA DUNIA

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohammed Mchengerwa, ameipongeza Kampuni ya Coca Cola Tanzania kwa kufanikisha ziara ya Kombe Halisi la Dunia la Fifa, huku akisema hafla ya Watanzania kupiga picha na kombe hilo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, itaambatana na uonyeshwaji wa Filamu ya Royal Tour.

**Royal Tour ni filamu iliyorekodiwa na Rais Samia Suluhu Hassan, ikitangaza utalii na vivutio vilivyopakaa Tanzania na kwamba kutokana na macho ya wadau wa soka duniani kuelekezwa nchini kutokana na ziara hiyo, basi ni fursa kwa Watanzania kujitokeza si tu kupiga nalo picha, bali kuona ubunifu wa rais katika filamu hiyo.**

Kombe la Dunia la FIFA limewasili nchini jana alfajiri, kabla ya kufanyika utambulisho kwa wanahabari katika hafla iliyofanyika Hyatt Regency Hotel na baadaye kupelekwa Ikulu ya Dar es Salaam, lilikopokelewa na Rais Samia - Mtanzania pekee anayeruhusiwa kulishika kwa mujibu wa Sheria za Fifa kuelekea Fainali za Kombe la Dunia Desemba mwaka huu nchini Qatar.

Taji hilo limetua nchini kwa msafara unaoongozwa na Juliano Belleti, beki wa zamani klabu kadhaa Ulaya zikiwamo Villareal, Barcelona (Hispania) na Chelsea ya Uingereza, ambaye alitwaa taji hilo akiwa timu ya Taifa ya Brazil katika fainali za Korea Kusini na Japan, mwaka 2002, ambako alikiri furaha kubwa kufika Tanzania.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo ya utambulisho wa ujio, Waziri Mchengerwa awali alisema kilichofanywa na Coca Cola Tanzania - kufanikisha ujio wa taji hilo ni jambo la kupongezwa, wao kama serikali wanaunga mkono jitihada hizo na wataitumia ziara hiyo kuongeza uwekezaji katika sekta ya michezo ili kuharakisha ukuaji wake.

"Kesho (leo) Juni Mosi itakuwa fursa muhimu kwa Watanzania kupiga nalo picha kuanzia saa tatu asubuhi hadi saa 11 jioni. Aidha, kutakuwa pia na onyesho la Filamu ya Royal Tour ya Rais Samia kuanzia saa 11 hadi saa 12. Kwa hiyo wito wetu kwa Watanzania kujitokeza kwa wingi kuja kuona matukio hayo mawili makubwa," alisema Mchengerwa.

Tanzania inahitimisha ziara ya taji hilo kwa nchi ambazo hazijafuzu fainali za Kombe la Dunia 2022 nchini Qatar, ambapo Afrika ziliteuliwa nchi nne tu, zikiwamo Ethiopia, Kenya na Afrika Kusini, na baada ya hapo, taji hilo litaanza ziara katika mataifa 32 yaliyofuzu fainali za Qatar, zikiwamo tano za Afrika.

Mkurugenzi Mkazi wa Coca Cola Kanda ya Tanzania, Hellen Masumba, alisema subira ya miaka nane kwa Watanzania kusubiri ziara ya zawadi kubwa na ya thamani zaidi duniani ya Kombe la Dunia, hatimaye kiu hiyo imekatwa kwa ziara hiyo, ambayo mara ya mwisho ilifanyika mwaka 2013, na kuonyeshwa dimbani CCM Kirumba jijini Mwanza.

"Nina furaha kuwajuza kuwa taji limetua nchini kwa jitihada za Coca Cola. Hii ni fursa kwa Watanzania kujumuika na wanamichezo hasa soka duniani kote, kwani ujio huu unafuatiliwa kote. Nichukue fursa hii kuwakaribisha Benjamin Mkapa kesho (leo) ili kupiga nalo picha na kujiwekea kumbukumbu ya kudumu maishani," alisema Hellen.




Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa (wapili kushoto) na mchezaji wa zamani wa Timu ya Taifa ya Brazil, Juliano Balletti (wapili kulia), wakiwa pamoja katika hafla ya utambulisho wa ujio wa Kombe la Dunia nchini iliyofanyika Hoteli ya Hyatt Kilimanjaro jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi Mkazi wa Coca Cola Kanda ya Tanzania, Hellen Masumba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Yanga yapania kutangaza ubingwa kwa Coastal*

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI kikosi cha Yanga kikitarajiwa kurudi kambini kesho, Kocha Msaidizi wa Klabu hiyo, Cedric Kaze, amesema mchezo wao dhidi ya Coastal Union ya Tanga wanatarajia utakuwa maalum kwa ajili ya kutangaza ubingwa wao msimu huu.

Yanga itaikaribisha Coastal Union Uwanja wa Benjamin Mkapa Juni 15, mwaka huu, na endapo itashinda itafikisha pointi 67 ambazo haziwezi kufikiwa na timu yoyote kwenye ligi hiyo msimu huu, huku ikiwa imebakiza mechi tatu.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, kocha huyo alisema mchezo huo ni muhimu kwao kwani wanakwenda kutangaza ubingwa endapo watashinda, hivyo kukata kiu yao ya kukaa muda mrefu bila kubeba taji hilo.

"Timu itaingia kambini Alhamisi (kesho) kwa ajili ya kuanza mikakati ya mchezo dhidi ya Coastal Union, tunaomba hata wale mashabiki ambao hawapendi kuja uwanjani siku hiyo waje kuona tunavyotangaza ubingwa wetu," alisema Kaze.

Alisema baada ya kurudi kambini, licha ya kwamba watakuwa na wachezaji pungufu kutokana na baadhi kuwa kwenye majukumu ya timu zao za Taifa, moja kwa moja wataanza mikakati yao hiyo.

Alisema anashukuru wameweza kuingia hatua ya fainali katika mashindano ya Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC) maarufu FA Cup, baada ya kumtoa mpinzani wao, Simba.

# Michezo

Jumatano Juni 1, 2022

Nipashe




Lewandowski amtibua Kahn Bayern UKURASA 21

# Rais Samia kusaidia AFCON 2027 kupigwa TZ

**Apokea Kombe la Dunia, Ikulu Dar, aahidi kupigana kupata viwanja vitatu vikubwa ili...**

**Na Saada Akida**

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, amesema atakuwa mstari wa mbele kuhakikisha Tanzania inatimiza vigezo vya kupata viwanja sita vitakavyokidhi kupewa uwenyeji wa Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) mwaka 2027.

**Kauli hiyo aliitoa Ikulu jijini Dar es Salaam jana wakati wa hafla ya kupokea Kombe la Dunia, ambayo alikuwa mgeni rasmi wa shughuli hiyo itakayoendelea leo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa Watanzania wote watakaojitokeza kupata fursa ya kupiga nalo picha.**

Rais Samia alisema ili kupata nafasi ya kuandaa michuano ya Afcon 2027, lazima Tanzania iwe na viwanja sita huku tayari ikiwa na vitatu ambavyo alivitaja kuwa ni Benjamini Mkapa, Uhuru vilivyopo Dar es salaam na Uwanja wa Amaan ulioko visiwani Zanzibar.

"Ili tufanye mashindano hayo ya AFCON lazima tuwe na viwanja sita vyenye sifa hadi sasa tunavyo vitatu, tunatakiwa kupata vitatu vingine, kwa hali hiyo nitakuwa bega kwa bega na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhakikisha tunapata viwanja vingine," alisema na kuongeza;

"Hadi sasa tayari tumeshakuwa na uhakika wa kupata uwanja mmoja baada ya kampuni mbili ikiwamo Coca Cola na nyingine kusaidia mchakato wa kupata uwanja wa nne, lakini tunatakiwa kupata hoteli na miundombinu ili tuwe wenyeji wa mashindano ya AFCON 2027."

Rais alisema anaipongeza Wizara ya Michezo kwa kupambana na kuhakikisha inapata nafasi ya kuwa mwenyeji wa mkutano wa CAF, utakaofanyika Agosti mwaka huu na kuitaka waitumie fursa hiyo kutangaza nchi na biashara kwa kuwalisha wageni vyakula vya Kitanzania.

"Ningependa kuwapo katika mkutano huo utakaokutanisha viongozi wa soka wa CAF, FIFA na viongozi wa nyama vya soka, tuombe kati ya hizo tarehe nisiwe na majukumu mengine," alisema Rais Samia.

Alisema ujio wa Kombe la Dunia nchini unapaswa kuwa chachu kwa wachezaji na wadau wa soka kufanya vizuri zaidi katika mchezo wa mpira wa miguu.

"Hii ni siku ya kipekee kwa kupokea Kombe la Dunia, nimefurahi kumuona Juliano Belleti, amewahi kutwaa Kombe la Dunia (akiwa na Brazil), nimefurahi kuona kabla ya kwenda Qatar kombe limepita hapa.

"Timu za wanawake na vijana zimekuwa zikifanya vema katika michezo, lakini umaliziaji umekuwa duni kombe hili linapaswa kututia moyo na kuwatayarisha vijana wetu kufanya vyema," alisema.

"Kama nchi tumefurahi kupokea kombe hilo na ninawaomba vijana wajitokeze kwa wingi ili waweze kutazama na kupiga picha," alisema Rais Samia.

Naye Mkurugenzi wa Coca Cola Kwanza, Unguu Suley, alisema kuwa Coca Cola, wanatoa shukrani zao kwa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kukubali kuwa mwenyeji na kulipokea Kombe la Dunia.

"Hii ni historia muhimu kwetu ikiwa ni miaka nane imepita baada ya Kombe la Dunia kuja hapa nchini huku ukiwa rais wa kwanza mwanamke kulipokea kombe hili, kwani katika kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wako kuna mafanikio mengi kwenye mchezo wa soka," alisema Suley.

LIMETUA...



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, akinyanyua juu Kombe la Dunia (World Cup), litakaloshindaniwa katika Fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika nchini Qatar baadaye mwaka huu katika hafla iliyofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Simba yamtimua Pablo, akataa kupokea barua

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imeamua kuachana na Kocha Mkuu wake, Pablo Franco raia wa Hispania, baada ya kuifundisha timu hiyo kwa muda wa miezi sita.

Pablo amekiri kupokea barua hiyo, lakini hakuisaini ili kukubali kwani kuna vitu ndani ya barua hiyo havijakaa sawa.

"Ni kweli tulikuwa na kikao na mabosi wangu, kuna mambo sikukubaliana nayo hususan upande wa usajili, jioni CEO alinitumia barua ya kuvunja mkataba, lakini ilikuwa na upungufu, hivyo sikusaini nilimrudishia ili arekebishe, ninachosubiri ni kufanyika kwa marekebisho hayo ili nisaini kukubali," alisema Pablo.

Kocha huyo ambaye alianza kuifundisha timu hiyo kuanzia Novemba mwaka jana, alisema hakupanga kuondoka kwenye klabu hiyo kwani tayari alikuwa ameshawakatia familia yake vibali vya kuishi nchini.

"Sikupanga kuondoka Simba kwani tayari nilikuwa nimeikatia Visa familia yangu ya kuishi hapa kwa mwaka mmoja, hivyo nasubiri akirekebisha hiyo barua na kuyaweka yale niliyoyapendekeza ambayo ni maslahi, basi nitasaini kuvunja mkataba," alisema Pablo.

Kwenye mtandao wake wa kijamii wa Instagram jana mchana, Simba ilitoa taarifa iliyosainiwa na Ofisa Mtendaji Mkuu, Barbara Gonzalez ambayo ilisema imefikia makubaliano ya pande zote mbili kuvunja mkataba na kocha huyo.

"Katika kipindi chake Kocha Pablo ameiwezesha timu yetu kutwaa Kombe la Mapinduzi na kufikia robo fainali ya Kombe la Shirikisho barani Afrika. Uongozi wa klabu ya Simba unamshukuru Kocha Pablo kwa mchango wake ndani ya klabu yetu," ilisema taarifa hiyo.

Mbali na kocha huyo pia imeachana na Kocha wa viungo, Daniel De Castro Reyes.

"Klabu inawatakiwa kila la kheri Kocha Pablo na mtaalamu wa viungo Daniel katika majukumu yao mapya, katika kipindi chote cha kumalizia msimu kikosi kitakuwa chini ya Kocha Msaidizi Selemani Matola." Iliendelea taarifa hiyo kwa umma.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >